# MATUMIZI YA MANENO YA BIBLIA KATIKA RIWAYA YA ROSA MISTIKA NA GAMBA LA NYOKA ZA EUPHRASE KEZILAHABI

**FERNANDES FRANCIS MAYO**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA(SEHEMU YA) MASHARTI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI (FASIHI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**FEBRUARI 2020**

## UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii iitwayo**"Matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka"*za Euphrase Kezilahabi** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili kukamilisha sehemu ya masharti ya Shahada ya Umahiri katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**..........................................................**

Dkt Hilda Pembe

**(Msimamizi)**

**..........................................................**

**Tarehe**

**IKIRARI NA HAKIMILIKI**

Mimi **Fernandes Francis Mayo,** ninathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa na mtu mwingine yeyote katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya kutunukiwa digrii nyingine yeyote.

Saini................................................ Tarehe.............................................

Haki ya kumiliki tasnifu hii inalindwa na mkataba wa Berne, sheria ya Haki kunakili ya mwaka 1999 na mikataba mingine ya kitaifa na kimataifa inayolinda mali za kitaaluma. Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yeyote ile, iwe ama yote au sehemu ya tasnifu hii, isipokuwa kwa shughuli halali, kwa ajili ya tafiti, kujisomea au kufanya marejeleo ya kitaaluma bila ya kibali cha maandishi ya Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

# TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mke wangu Judith,mama yangu Ancila, na wanangu Ancila, Francis, Hellen na Fransisca.

## SHUKURANI

Namshukuru mwenyezi Mungu kwa kunilinda, kunipigania na kunipa uzima na afya tele hadi kuweza kufikia katika kiwango hiki cha elimu.

Kukamilika kwa kazi hii kumetokana na michango ya watu mbalimbali ambao walishirikiana nami bega kwa bega kwa viwango tofauti. Sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwa watu hao. Kwa kuwa ni vigumu kuwataja wote, nitataja wachache tu kwa niaba ya wote kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, ninapenda kumshukuru msimamizi wangu Dkt. Hilda Pembe kwa upole, ukarimu, hekima na busara zake kwa kuwa nami katika kila hatua ili kuhakikisha kazi hii inakuwa katika kiwango chenye ubora. Licha ya kuwa na majukumu mengi, hakusita kunipa miongozo ya kuboresha kazi hii.

Pili, niwashukuru wahadhiri wote wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania wakiwemo Prof. Emmanuel Mbogo, Dkt. Mohammed Maguo, na Dkt Zelda Elisifa kwa kunipa maarifa ambayo yamechangia kuweza kuandika kazi hii. Pia, niwashukuru wafanyakazi wote wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, tawi la Arusha kwa ushirikiano wao walionionesha wakati wa masomo yangu na wakati wote wa uandishi wa Tasnifu hii. Vilevile ninawashukuru wanafunzi wenzangu tuliosoma nao kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha masomo ambao ni Bw. Gerson Mrua, Bi. Georgia Maghiya, Bi. Upendo Shayo na Bw. Meijo Laizer.

# YALIYOMO

Uthibitisho....................................................................................................ii

Ikirari na hakimiliki....................................................................................................iii

Tabaruku....................................................................................................iv

Shukurani....................................................................................................v

Yaliyomo .......vi

Orodha ya majedwali....................................................................................................x

Orodha ya vifupisho....................................................................................................xi

Ikisiri....................................................................................................xii

**SURA YA KWANZA: MISINGI YA UTAFITI....................................................................1**

1.0 Utangulizi....................................................................................................1

1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti....................................................................................................1

1.2 Tatizo la Utafiti....................................................................................................4

1.3 Lengo la Utafiti....................................................................................................5

1.3.1 Malengo Mahususi....................................................................................................5

1.4 Maswali ya Utafiti....................................................................................................5

1.5 Umuhimu wa Utafiti....................................................................................................6

1.6 Mipaka ya Utafiti....................................................................................................6

1.7 Mpangilio wa Tasnifu....................................................................................................7

**SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA........8**

2.0 Utangulizi....................................................................................................8

2.1 Historia Fupi ya Euphrase Kezilahabi....................................................................................................8

2.1.1 Muhtasari wa Riwaya ya Rosa *Mistika* ..................................................................11

2.1.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Gamba la Nyoka*..............................................................12

2.2 Dhana ya Riwaya..........................................................................................................13

2.2.1 Aina za Riwaya............................................................................................................14

2.2.2 Uainishaji wa Riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka*....................................20

2.3 Tafiti Zinazohusiana na Riwaya za Euphrase Kezilahabi...........................................21

2.4 Dhana ya Dini...............................................................................................................24

2.5 Tafiti Zihusuzo Dini......................................................................................................25

2.6 Kiunzi cha Nadharia.....................................................................................................27

2.7 Pengo la Utafiti.............................................................................................................30

2.8 Hitimisho......................................................................................................................31

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI.......................................................................32**

3.0 Utangulizi......................................................................................................................32

3.1 Muundo wa Utafiti........................................................................................................32

3.2 Eneo la Utafiti...............................................................................................................33

3.3 Sampuli na Usampulishaji............................................................................................33

3.4 Mbinu za Ukusanyaji Data...........................................................................................35

3.5 Zana za Utafiti..............................................................................................................36

3.5.1 Kalamu na Shajara......................................................................................................36

3.5.2 Ngamizi.......................................................................................................................37

3.5.3 Kihifadhi Data Nje......................................................................................................37

3.5.4 Kinyonyi......................................................................................................................37

3.6 Uchambuzi na Uwasilishaji wa Data.....38

3.7 Uthabiti, Kuaminika na Maadili ya Utafiti.....39

3.7.1 Uthabiti wa Data.....39

3.7.2 Kuaminika kwa Utafiti.....39

3.7.3 Maadili ya Utafiti.....40

3.8 Changamoto za Utafiti.....40

3.9 Hitimisho.....40

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI.....42**

4.0 Utangulizi.....42

4.1 Matumizi ya Maneno ya Biblia katika Riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka*.....42

4.1.1 Matumizi ya Maneno ya Biblia katika Riwaya ya *Rosa Mistika*.....44

4.1.1.1 Kunyweni hii ndio damu yangu......44

4.1.1.2 Maskini wa Roho.....46

4.1.1.3 Kuungama Dhambi.....47

4.1.1.4 Kiti cha Enzi.....50

4.1.1.5 Utakatifu.....52

4.1.2 Matumizi ya Maneno ya Biblia katika Riwaya ya *Gamba la Nyoka*.....54

4.1.2.1 Damu yao na iwe juu ya vichwa vyenu, mimi nanawa mikono kama Pilato.....54

4.1.2.2 Baba ikiwezekana kikombe hiki kinipite.....56

4.1.2.3 Kwa Jina la Baba, na Mwana na la Roho Mtakatifu.....57

4.1.2.4 Maria, mama wa Mungu aliyezaa kwa nguvu za Roho Mtakatifu........................59

4.2 Dhima za Matumizi ya Maneno ya Biblia katika Riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka*.......................................................................................................60

4.2.1 Kulea watu Kiroho.......................................................................................61

4.2.2 Kejeli..........................................................................................................63

4.2.3 Kukata Tamaa.............................................................................................64

4.2.4 Unafiki wa Viongozi wa Dini.......................................................................67

4.3 Athari za Matumizi ya Maneno ya Biblia kwa Wakristo..........................................69

4.3.1 Kutokuwa na Imani na Viongozi wa Dini..........................................................70

4.3.2 Kurudisha Maendeleo Nyuma........................................................................72

4.4 Hitimisho.........................................................................................................73

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.................74**

5.0 Utangulizi.......................................................................................................74

5.1 Muhtasari........................................................................................................74

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti……………………………………………………75

5.3 Hitimisho.........................................................................................................75

5.4 Mapendekezo....................................................................................................76

5.4.1 Mapendekezo kwa ajili ya uboreshaji wa Utafiti.................................................77

5.4.2 Mapendekezo ya Tafiti Nyingine.....................................................................77

Marejeo...............................................................................................................78

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 4.1: Idadi ya maneno ya Biblia yaliyotumika katika Riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka*..........................................................................................................43

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BAKITA | Baraza la Kiswahili la Taifa. |
| Prof | Profesa. |
| DKT | Daktari. |
| Uk | Ukurasa. |
| Bw | Bwana. |
| Bi | Bibi. |
| Ktj | Keshatajwa |
| Ht | Hakuna Tarehe |

# IKISIRI

Utafiti huu unahusu matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka*. Utafiti huu umeongozwa na malengo matatu ambayo ni kubainisha maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka*, kueleza dhima za matumizi ya maneno hayo na kubaini athari za matumizi ya maneno ya Biblia kwa Wakristo ukiongozwa na nadharia ya Uhemenitiki. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya upekuzi matini nakuwasilishwa kwa kutumia mkabala wa kiidadi na kimaelezo. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwepo kwa matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya hizo kama vile Kunyweni hii ndio damu yangu, Maskini wa roho, Kuungama dhambi, Kiti cha enzi, Utakatifu, Damu yao na iwe juu ya vichwa vyenu mimi ninanawa mikono kama Pilato, Baba ikiwezekana kikombe hiki kinipite, Kwa jina la Baba, na Mwana na la Roho Mtakatifu, na Maria, mama wa Mungu aliyezaa kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Aidha, zipo dhima mbalimbali zilizojitokeza kama vile kulea watu kiroho, kukejeli, kufariji watu waliokata tamaa na kuonesha unafiki wa viongozi wa dini.Halikadhalika, zipo athari ambazo zimeonekana ambazo ni kutokuwa na imani na viongozi wa dini pamoja na kurudisha maendeleo nyuma. Kutokana na matokeo ya utafiti huu tunapendekeza kwamba, utafiti mwingine unaweza kufanywa kwa kuangalia matumizi ya maneno ya Biblia katika tanzu nyingine za fasihi kama vile tamthiliya, ushairi pamoja na fasihi simulizi.

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea misingi ya utafiti. Sura imegawanyika katika sehemu nane ambapo sehemu ya kwanza imeelezea usuli wa tatizo, sehemu ya pili imeelezea tatizo la utafiti ilhali sehemu ya tatu imeangazia malengo ya utafiti. Aidha sehemu ya nne imetaja maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti umejadiliwa sehemu ya tano na mipaka ya utafiti imejadiliwa sehemu ya sita. Sehemu ya saba imefafanua uchanganuzi wa data na sehemu ya nane ni mpangilio wa utafiti ambao ndilo hitimisho la sura hii.

## 1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Suala la imani ni jambo ambalo kila mtu ana uhuru binafsi wa kuamua aingie katika imani ipi ambayo kwa mtazamo wake anaona itamjenga na kumkuza kiroho katika misingi inayofaa. BAKITA (2016:327) inaeleza kuwa imani ni fikra za mtu juu ya maisha yanayomfanya awe na mtazamo fulani anaoufuata. Imani inamfanya mtu kuamini au kukubali kuwa kitu fulani kipo na ni kweli bila ya uthibitisho. Pembe (Ht) anaeleza kwamba, kila mtu ana imani tofauti na mwenzake na kwamba Watanzania wameathiriwa na dini ya Uislamu na Ukristo ingawa wapo wachache wanaoamini katika dini za Kihindi na imani za kiasili za Afrika. Kutokana na mazingira hayo, kila dini huwa na kanuni na taratibu fulani za kuabudu ambazo zinatofautiana na dini nyingine. Kwa mfano dini za Uislamu na Ukristo zinatofautiana katika vipengele vya kuzika, mkao wa waumini ndani

ya ibada, mtume wanayepitia katika kuabudu, utoaji majina pamoja na mavazi. Pamoja na tofauti hizo, waumini wote wa Kiislamu na Kikristo hatima yao ni kumwabudu Mwenyezi Mungu. Utofauti huo unaweza kuwafanya watu wengine wakafurahishwa au kutofurahishwa na dini nyingine.

Wakristo wanatumia Biblia kuendeleza imani yao halikadhalika Waislam wanatumia Kuruani. Msangi (2018) anafafanua kuwa Biblia ni kitabu Kitakatifu wanachokitumia Wakristo kukuza imani yao ilhali Kuruani ni kitabu Kitakatifu wanachotumia Waislam kukuza imani yao. Vitabu vyote hivi vitakatifu ni muhimu kwa wanajamii kutokana na kwamba vinahubiri amani, upendo, umoja, mshikamano, heshima, utu wema na fadhili.
Fasihi ni sanaa inayobuniwa ili kuakisi hali halisi katika jamii husika. Matukio yanayoshuhudiwa huwasilishwa kwa ubunifu katika muktadha wa utamaduni na historia ya jamii kupitia fasihi simulizi au fasihi andishi. Kupitia matukio mbalimbali ya kiimani, kiitikadi, busara na falsafa ya watu fasihi huweza kufafanuliwa na kuwasilishwa katika jamii husika. Fasihi andishi huwasilishwa kwa maandishi na ina tanzu kuu tatu ambazo ni ushairi, tamthilia na riwaya. Tanzu hizi, huwasilisha matukio mbalimbali ya kijamii ikiwemo hisi na mielekeo ya kiimani na kiitikadi inayotokana na tajiriba ya watu katika mazingira ya utamaduni wao. Ni kwa maana hiyo ambapo utanzu wa riwaya ya Kiswahili unadhihirisha namna unavyowasilisha maudhui ya kiimani yaani imani ya Kikristo au Kiislam katika matumizi ya maneno mbalimbali wakati wa uwasilishaji wa ujumbe katika jamii.

Riwaya ni miongoni mwa tanzu ya fasihi andishi inayotumia lugha ya nadharia katika masimulizi yake yanayoweza kuwa ama ya kweli au ya kubuni. Katika fasihi andishi utanzu wa riwaya ndio utanzu ulioibuka hivi karibuni ukilinganisha na tanzu za tamthiliya na ushairi (Senkoro, 2011). Senkoro (ktj) anaendelea kudai kuwa utanzu wa riwaya uliibuka kutokana na maendeleo na mageuzi ya kitamaduni na viwanda. Maendeleo na mageuzi haya yalihitaji kuwa na utanzu wa fasihi andishi ulio na uchangamano kifani na kimaudhui ili kukidhi haja ya kuelezwa kwa mawanda mapana kutokana na mchanganyiko wa maisha ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

Wataalamu wengi wamejadili sifa mbalimbali za riwaya ya Kiswahili kama vile kutumia wahusika wengi, matukio kuingiliana hata kusababisha kuwa na hadithi ndani ya hadithi, matumizi ya taharuki kubwa, matukio huelezwa kwa uzito na upana wa kutosha na muundo wake huwa ama wa msago au kioo (Msokile, 1992; Madumulla, 2009 na Senkoro, 2011).

Riwaya husawiri maisha ya jamii yaliyotokea au yanayoweza kutokea. Imani kama moja ya itikadi inayomfanya mtu kuamini kitu fulani huweza kuwasilishwa kupitia kazi ya fasihi. Kwa mujibu wa Pembe (2017) waandishi kama vile Euphrase Kezilahabi, Said Mohamed, Ebrahim Hussein, Ben Mtobwa na Penina Mlama katika kazi zao za fasihi wameathiriwa na dini, tamaduni, mazingira na historia. Kwa mfano, mwandishi Euphrase Kezilahabi amekulia katika mazingira ya dini ya Kikristo dhehebu la Katoliki pamoja na utamaduni wa Kikerewe, hivyo majina ya wahusika na matukio yake katika kazi zake

mbalimbali za fasihi husawiri dini ya Kikristo hususani imani ya Katoliki pamoja na tamaduni za Kikerewe.

Hivyo, kupitia matumizi ya maneno ya Biblia katika uandishi wa kazi za fasihi unadhihirisha imani aliyonayo mwandishi Euphrase Kezilahabi juu ya kuwako na kutokuwako kwa Mungu. Aidha, mwandishi anatambua mchango wa dini katika kumuongoza mwanadamu katika harakati za kutafuta kiini na maana ya maisha. Hali kadhalika, katika kutambua umuhimu wa dini katika kumuongoza mwanadamu, mwandishi anaona binadamu anaishia katika matatizo kadha wa kadha, ikiwa ni pamoja na kukata tamaa ya maisha na kujikuta katika misukosuko ya maisha. Hali hii imemsababisha kuandika riwaya zake kwa kuegemea mkondo wa mawazo ya kidhanaishi na kutumia maneno ya Biblia katika vitabu vyake ili kuweza kudhihirisha imani yake.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Mwandishi wa riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka* Euphrase Kezilahabi, ametumia mbinu mbalimbali katika kuhakikisha kwamba jamii inafikiwa na ujumbe kama alivyokusudia. Kipengele hiki cha lugha kama mbinu mojawapo ya uandishi huwa na nafasi kubwa katika kufanikisha ujumbe uliokusudiwa na mwandishi kufikia jamii husika. Hata hivyo, lugha ikitumika vibaya inaweza kukwamisha ujumbe. Mwandishi Euphrase Kezilahabi katika kufikisha ujumbe katika jamii ametumia maneno kadhaa yaliyojikita katika msingi wa imani ya Kikristo hususani dhehebu la Katoliki. Kiujumla maneno yanapotumika katika miktadha mbalimbali huibua athari na mitazamo tofauti

tofauti kwa jamii husika. Hivyo, utafiti huu ulikusudia kuchunguza maneno ya Biblia katika riwaya za *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka* na iwapo kuna athari zozote za utumizi wa maneno hayo katika jamii.

## 1.3 Lengo la Utafiti

Utafiti huu unalengakuchunguza matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika*na*Gamba la Nyoka* zilizoandikwa na Euphrase Kezilahabi.

### 1.3.1 Malengo Mahususi

Utafiti huu umeongozwa na malengo mahususi yafuatayo:-

(i) Kubainisha matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka*.

(ii) Kueleza dhima za matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka*.

(iii) Kubaini athari za maneno ya Biblia yaliyotumika katika riwaya ya *RosaMistika* na *Gamba la Nyoka.*

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maswali yafuatayo:-

(i) Je, kuna matumizigani ya maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka?*

(ii) Je, zipi dhima za matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka?*

(iii) Je, maneno ya Biblia yaliyotumika katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka* yana athari gani kwa Wakristo?

**1.5 Umuhimu wa Utafiti**

Koul (2009) anabainisha kuwa umuhimu wa utafiti ni ile thamani yake na kuhitajika kwa uchunguzi wa jambo kwa wakati husika. Kwa minajili hiyo, utafiti huu utatumika kama marejeleo katika taaluma ya fasihi na kwa maana hiyo, utawasaidia wanafunzi na watafiti wengine kupata maarifa mbalimbali ya fasihi na imani ya Kikristo.

Vile vile, utafiti huu utakuwa ni changamoto kwa watafiti wengine kufanya utafiti katika tanzu nyingine za fasihi kama vile tamthilia na ushairi katika kipengele cha matumizi ya maneno ya Biblia au hata ya Kuruani Takatifu.

**1.6 Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu umejikita katika kuchunguza maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* na*Gamba la Nyoka*. Maneno mengine ambayo si ya Biblia hayajahusishwa katika utafiti huu japo yamerejelewa kwa namna moja au nyingine kama moja ya marejeo.

Mwandishi ameandika vitabu vingi vya riwaya, ushairi na tamthiliya, lakini utafiti huu umejikita katika kuchunguza matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka.* Tanzu ya ushairi na tamthilia hazijahusishwa katika utafiti

huu. Aidha riwaya nyingine ambazo si teule hazijahusishwa pia katika utafiti huu japokuwa zimerejelewa kwa namna moja au nyingine kama moja ya marejeo katika ufafanuzi wa kazi za Euphrase Kezilahabi.

### 1.7 Mpangilio wa Tasnifu

Utafiti huu una sura tano. Sura ya kwanza ni misingi ya utafiti ambapo vipengele mbalimbali vimejadiliwa kama vile usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasnifu.

Sura ya pili imejengwa na mapitio ya maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada husika Sura imegawanyika katika sehemu sita. Sehemu ya kwanza imejadili historia fupi ya Euphrase Kezilahabi, sehemu ya pili imeeleza dhana ya riwaya, sehemu ya tatu imeangazia tafiti zinazohusiana na riwaya za Euphrase Kezilahabi, sehemu ya nne imejadili dhana ya dini halikadhalika sehemu ya tano imejadili tafiti zinazohusiana na dini. Kiunzi cha nadharia kilichotumika katika uchambuzi wa data kimejadiliwa sehemu ya sita.

Sehemu ya tatu imejadili mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Vipengele viliyozungumziwa ni pamoja na muundo wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za ukusanyaji data, zana za utafiti, uchambuzi wa data, uthabiti, kuaminika na maadili ya utafiti pamoja na changamoto za utafiti zimejadiliwa pia. Aidha sura ya nne imejadili uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti pamoja na hitimisho.

Sura ya tano imezungumzia muhtasari wa utafiti, hitimisho na mapendekezo.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inaeleza mapitio ya maandiko pamoja na kiunzi cha nadharia. Sura imegawanyika katika sehemu sita. Sehemu ya kwanza imejadili historia fupi ya Euphrase Kezilahabi, sehemu ya pili imeeleza dhana ya riwaya, sehemu ya tatu imeangazia tafiti zinazohusiana na riwaya za Euphrase Kezilahabi, sehemu ya nne imejadili dhana ya dini halikadhalika sehemu ya tano imejadili tafiti zinazohusu dini. Kiunzi cha nadharia kilichotumika katika uchambuzi wa data kimejadiliwa sehemu ya sita.

## 2.1 Historia Fupi ya Euphrase Kezilahabi

Mwandishi mashuhuri na mwanafalsafa wa fasihi ya Kiswahili, Euphrase Kezilahabi alizaliwa Aprili 13, 1944 katika kijiji cha Namagondo kisiwa cha Ukerewe mkoani Mwanza. Euphrase Kezilahabi alisoma shule ya msingi Nakasayenge na kuendelea na masomo ya sekondari katika seminari ya Katoliki Nyegezi. Mwaka 1967 alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kupata Shahada ya kwanza katika elimu, lugha na fasihi. Hata hivyo, aliendelea na masomo ya Shahada ya Umahiri na Uzamivu katika Chuo Kikuu cha Wisconcin-Madison nchini Marekani na kuhitimu mwaka 1985. Euphrase Kezilahabi amefanya kazi ya ufundishaji katika shule za sekondari ya Mzumbe na Mkwawa na pia kufundisha katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama Mhadhiri Mwandamizi. Euphrase Kezilahabi ameandika kazi mbalimbaliza kifasihi zikiwemo

riwaya na ushairi zilizoegemea katika mkondo wa udhanaishi. Baadhi ya kazi zake ni*Rosa Mistika (1971), Kichwa maji (1974), Dunia uwanja wa Fujo (1975), Gamba la Nyoka (1979), Nagona (1990), Mzingile (1991).* Vilevile ameandika diwani kama vile *Kichomi (1974), Karibu Ndani (1988)* na *Dhifa (2008).* Aidha, ameandika tamthiliya ya *Kaptula la Marx (1978).*Kwa sasa Euphrase Kezilahabi ni Profesa wa lugha za Kiafrika kwenye Chuo Kikuu cha Botswana tangu mwaka 2012. Kupitia historia hii, Senkoro (1995) anaongezea kuwa, maisha ya kiimani ya Euphrase Kezilahabi na kusoma seminari imemuathiri Euphrase Kezilahabi kwa kiasi kikubwa katika uandishi wa kazi zake za kifasihi.

Euphrase Kezilahabi amepata sifa ya kutambulika kama mwanasanaa wa kiwango cha juu katika kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili (Wamitila 2002). Ustadi wake umejikita katika matumizi ya maneno ya Bibliana ishara huku mada zake zikielemea katika masuala ya kimetafizikia yahusuyo maisha, kifo, furaha na ukweli. Euphrase Kezilahabi ni miongoni mwa waandishi waliokuja na mbinu mpya za uandishi wa ushairi ulioibua mgogoro baina ya wanausasa na wanamapokeo (Mlaga, 2017). Hakuishia tu katika kueleza mtindo mpya lakini hata mada zake ziligusa maswala tata ya kiitikadi na ukanusho wa kuwepo kwa Mungu, maisha baada ya kifo, dini, nguvu za ujaala na kuungana na wanauyakinifu haswa mkondo wa Kidarwin katika kufasiri matukio na maisha ya binadamu(Wamitila 2002).

Euphrase Kezilahabini mtunzi wa kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili aliyeathiriwa na falsafa ya kidhanaishi ya Fredrick Nietzsche ambayo amekuwa akiitumia katika uandishi

wake wa kazi za fasihi kama vile riwaya yake ya pili ya *Kichwamaji* (1974) kupitia mhusika Kichwamaji. Kauli ya kuathiriwa na falsafa ya kidhanaishi inathibitishwa na Rehak (2007:136) pale alipobaini waziwazi kuwa riwaya ya *Kichwamaji* ni kazi ya kwanza inayobainisha udhanaishi katika fasihi ya Kiswahili. Si Rehak tu aliyethibitisha matumizi ya udhanaishi kwa mwandishi Euphrase Kezilahabi, bali hata Sakkos (2008) anaeleza kuwa riwaya ya *Kichwamaji* ni riwaya ya kwanza katika fasihi ya Kiswahili iliyotumia mawazo ya akina Albert Camus na Jean Paul Sartre waliokuwa ni waasisi wa nadharia ya udhanaishi.

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), Udhanaishi ni dhana inayojishughulisha zaidi na dhana ya maisha yaani nafasi ya mwanadamu ulimwenguni na uhusiano uliopo kati ya binadamu na Mungu. Naye Wanjala (2012) anaiweka wazi dhana ya udhanaishi kuwa ni falsafa au mtazamo wa maisha ulio na kitovu chake katika swali la maisha ni nini? Na yana maana gani kwa binadamu. Kwa ujumla dhana ya udhanaishi ni falsafa ambayo inamulika kwa kina masuala ya maudhui ya kifo, uhuru wa mtu binafsi, wajibu wa binadamu duniani, ubinafsi, kukata tamaa, udhaifu wa binadamu, furaha, ukengeushi na kuwepo au kutokuwepo kwa Mungu. Mtazamo huo ndio unaojitokeza pia kwa Wamitila (2003) anapoipambanua dhana hiyo ya udhanaishi kwa kubaini kwamba ni dhana inayotumiwa kueleza falsafa ya maisha.  Hivyo basi udhanaishi nimtazamo unaohusiana na hali ya maisha ya binadamu, nafasi na jukumu lake ulimwenguni na uhusiano wake na Mungu kutokuwepo.

### 2.1.1 Muhtasari wa Riwaya ya Rosa *Mistika*

Riwaya ya *Rosa Mistika* kwa kiasi kikubwa masimulizi yake yamejikita katika kueleza maisha ya mhusika Rosa tangu akiwa mtoto mpaka kifo chake na maisha baada ya kifo. Masimulizi yamehusisha maisha ya wahusika wengine ambao kimsingi ndio ambao wamemjenga mhusika mkuu Rosa. Wahusika hao ni Regina ambaye ni mama yake Rosa, Zakaria baba yake Rosa, Flora mdogo wake Rosa, Charles mpenzi wa Rosa na Padri anayetaka kuokoa nafsi ya Rosa. Rosa akiwa mtoto mdogo anaonekana ni msichana mrembo na mwenye aibu, mrefu kiasi, mnyenyekevu na mkakamavu.

Rosa anakuwa chini ya malezi ya baba yake aliye na mtazamo hasi juu ya wanawake. Zakaria akiwa kama mwalimu aliyeachishwa kazi kwa sababu ya ulevi, kutojali familia yake, kumtesa mke wake kwa kumpiga kwa sababu ya kuzaa watoto wa kike wengi. Ingawa Regina alipigwa na mumewe lakini hakutaka kuachana na mumewe sababu ya mategemeo yake juu ya maisha ya baadae ya watoto wake. Zakaria anashindwa kutafuta njia sahihi katika kuwalea binti zake. Hajui jinsi ya kukabiliana na Rosa aliye katika hatua muhimu katika makuzi yake. Zakaria hana muda wa kuzungumza na binti zake juu ya hisia zao wala hawaelezi namna ya kukabiliana nazo katika hatua hii ya makuzi.

Hivyo, Rosa anajikuta anaingia katika umalaya hadi kufukuzwa shule. Rosa anajikuta katika misukosuko ya maisha na kukata tamaa baada ya kuona kwamba ndoto ya kuolewa na mchumba wake Charles imezima baada ya Charles kumkuta hana bikira.

Hapo ndipo anapochukua hatua ya kujiua kwa kuona kwamba maisha yake hayana maana hapa duniani.

### 2.1.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Gamba la Nyoka*

*Gamba la Nyoka* ni riwaya inayoonesha jinsi maamuzi ya kisiasa yasiyotafakariwa yanavyoweza kuwa na athari mbaya kwa wanyonge. Riwaya inayotashititi sera zinazoongozwa na ubinafsi, kisasi na pupa ya utekelezaji. Mwandishi amewachora wahusika wa namna mbalimbali wenye kuwakilisha kundi la wasomi mfano Mambosasa na Mamboleo; kundi la wakulima mfano wanakijiji cha Buso na Kisole, kiongozi wa dini mfano Padri Madevu, viongozi wa aina mbalimbali kama Raisi, wakuu wa Wilaya, wenyeviti wa vijiji na maaskari. Mwandishi anazungumzia kuhusu mmomonyoko wa maadili kwa waumini na watumishi wa kanisa kwa kumtumia Padri Madevu kama mfano wa kumomonyoka kwa maadili ya viongozi wa kanisa, kwani inasawiriwa kuwa Padri Madevu anatembea na mjane na anatoa dawa za kuzuia mimba kitu ambacho ni kinyume na maadili ya Kanisa Katoliki. Aidha, mwandishi anatafakari kwa kina juu ya Kanisa Katoliki kuhusu Utatu Mtakatifu, Bikira Maria na hali ya ubikira hata baada ya kujifungua. Yote haya yanafanyika wakati akiisawiri historia ya Tanzania, hususani uanzishwaji wa vijiji vya ujamaa. Kwa ujumla riwaya hii inaelezea dhana nzima ya Ujamaa na vijiji vya Ujamaa pamoja na utekelezaji wake.

## 2.2 Dhana ya Riwaya

Matteru (1976) anafafanua kuwa riwaya ni hadithi ndefu ambazo zimeandikwa. Kutokana na maana hii tunaweza kuona mambo matatu makuu katika dhana ya riwaya, kwamba riwaya ni hadithi, hadithi ni lazima iwe ndefu na ni lazima iwe imeandikwa. Mphalale (1976) anasema, riwaya ni hadithi ndefu za maneno kati ya 35,000 na 50,000. Hii ina maana kwamba iwapo hadithi haitafikia idadi hiyo ya maneno basi haitaitwa riwaya bali itaitwa hadithi fupi. Mulokozi (1996) anaeleza kuwa riwaya ni kazi ambayo inakuwa na sifa mbali mbali kama vile kuwepo na ubunifu, usimulizi, mpangilio au msukumo fulani wa matukio (ploti), mfungamano wa wakati, visa vinatendeka katika wakati fulani, inatakiwa iwe na maneno mengi na itakapokuwa na maneno pungufu ya elfu tatu (3000), yaweza kuitwa Novela (hadithi fupi), pawepo na mawanda mapana (kwa upande wa yale yanayozungumzwa, wakati na mahali pa matukio hayo), na pia pawepo na uchangamani katika visa, dhamira, tabia na wahusika.

Chuachua (2011) anafasili kuwa riwaya ni kazi ya kubuni ya kinathari yenye uchangamani wa fikra, msuko, mandhari na uhusika unaomsawiri binadamu na maisha yake. Hii inaonesha kwamba tunapozungumzia uchangamani ni ile hali ya kuunda kazi kisanii kwa kutumia mbinu mbali mbali za kiubunifu (kiumbilizi) na ndipo unamfanya kumfikirisha msomaji na uchangamani ndio kigezo kikuu kinachotofautisha riwaya na aina nyingine za nathari. Hivyo basi, kwa kurejelea fasili za wataalamu mbalimbali dhana ya riwaya inaweza kuelezwa kwamba ni hadithi ndefu ya kubuni yenye visa vingi,

wahusika wengi, maandishi ya mjazo yenye kutoa maelezo yanayozungumzia kwa upana na urefu wa maisha ya jamii.

### 2.2.1 Aina za Riwaya

Kuna aina mbalimbali za riwaya kama alivyoainisha Madumulla (2009) pale anaposema ieleweke kuwa kuna aina kadhaa za riwaya kulingana na njia iliyochaguliwa na msimulizi. Riwaya huweza kuanishwa kifani, kidhamira, kimaudhui, kihistoria, na kiitikadi. Mulokozi (1996), Madumula (2009) na Wamitila (2002) wameainisha aina za riwaya kama ifuatavyo:-*riwaya ya kisaikolojia* ni aina ya riwaya inayododosa nafsi ya mhusika, fikra, hisia mawazo, imani, hofu, mashaka, matumaini na athari ya mambo hayo kwake binafsi na labda kwa jamii. Mfano wa riwaya ya kisaikolojia ni *Kichwa Maji (1974)* na *Rosa Mistika (1971)* za E. Kezilahabi; *Kiu (1985)* na *Nyota ya Rehema (1981) za* M.S. Mohammed. Pia kuna *riwaya ya kisosholojia au jamii* ni riwaya ambayo inasawiri maisha ya kawaida ya jamii kwa kuchunguza matatizo yake, yawe ya kifamilia, kitabaka, kiuchumi, kisiasa au hata kiutamaduni. Mfano wa riwaya ya kisosholojia ni *Titi la Mkwe* (1972) ya A. Banzi; *Kurwa na Doto (1960) ya* M.S. Farsi na *Dunia Uwanja wa Fujo (1975) ya* E. Kezilahabi. Vilevile kuna riwaya ya kihistoria ni aina ya riwaya ambayo msingi wake huhusu matukio fulani katika jamii ya mwandishi ambayo yanaleta historia ya tukio fulani. Tukio hilo huwa ni kubwa na la muhimu kijamii, laweza kuwa la kikabila au la kitaifa. Mfano wa riwaya ya kihistoria ni *Uhuru wa Watumwa (1934) ya* J. Mbotela; *Miradi Bubu ya Wazalendo* (1992) ya G. Ruhumbika na *Zawadi ya Ushindi* (1987) ya B. Mtobwa.

Riwaya ya uhalifu ni aina nyingine ya riwaya ambayo hujihusisha na uhalifu wa aina mbalimbali kama vile ujambazi, uuaji, magendo na utapeli. Mfano wa riwaya ya uhalifu ni *Kwa sababu ya Pesa (1972) ya* J.Simbamwene na *Sanda ya Jambazi* (1977) ya H. Rajab. Sambamba na aina hizo kuna riwaya ya upelelezi ambayo huwa na vitu viwili yaani uhalifu na upelelezi wa uhalifu hadi mhalifu anapopatikana. Hivyo wahusika wake ni wahalifu, wadhulumiwa na wapelelezi wakiwemo polisi. Mfano wa riwaya ya upelelezi ni *Mzimu wa Watu wa Kale (1960) ya* M.S. Abdulla na *Duniani kuna Watu* (1973) ya M.S. Abdulla. Aina nyingine ni riwaya ya barua ambayo huwa na muundo wa barua kuanzia mwanzo hadi mwisho wa riwaya, Mfano riwaya ya *Pamela (1749)* ya S.Richardson na *Barua Ndefu kama Hii (1979) ya* Mariam Ba.Aidha, riwaya ya vitisho ni riwaya yenye visa vya kusisimua damu na mara nyingi visa hivyo huambatana na matukio ya ajabu na miujiza, mfano riwaya ya *Mirathi ya Hatari (1977) ya* C. Mung'ong'o na *Vipuli vya Figo (1996) ya* E. Mbogo. Pia kuna riwaya ya majaribioni aina ya riwaya inayojadili mkondo mpya wa utunzi wa riwaya ambapo mjadala nafsi hutungwa bila kuzingatia kanuni za kawaida za uandishi wa riwaya. Watunzi wa riwaya ya majaribio hudai kuwa kumbo la kawaida la riwaya hautoshelezi mahitaji ya karne hii katika kuwakilisha ukweli wa maisha ya mwanadamu na hivyo kuna uhitaji wa kuwepo na aina nyingine ya riwaya itakayotimiza mahitaji yote. Mfano wa riwaya hizo ni *Hukumu ya Kasri* na *Bina-Adam (2002)* na *Musaleo (2004) za* W.K Wamitila.

Riwaya ya kitawasifuni aina nyingine ambayo ina muundo unafanana na muundo wa tawasifu kwa kuyachunguza maisha ya mtu fulani na hutumia nafsi ya kwanzakatika kuwasilisha ujumbe. Mfano riwaya ya *Uhuru wa watumwa (1934) ya* J. Mbotela na

*Maisha Yangu na baada ya Miaka Hamsini (1934) ya* S.Robert. Vilevile kunariwaya ya wasifu ambayo huzungumzia maisha ya mtu fulani. Mfano riwaya ya *Wasifu wa Siti Binti Saad (1967) ya* S. Robert. Mbali na riwaya hizo pia kuna riwaya ya kifalsafa ambayo inashughulikia masuala ya kifalsafa. Mada ya kifalsafa huchukua sehemu muhimu katika riwaya ya aina hii kuliko wahusika, mandhari, msuko au mtukio. Mfano riwaya ya *Nagona (1990) na Mzingile (1991) za* E. Kezilahabi. Pia kuna riwaya ya mapenzi, aina hii yariwaya kusawiri uhusiano wa kimapenzi kati ya mvulana na msichana. Mfano riwaya ya *Rais anampenda mke wangu* (2003) ya E.Shigongo na*Kweli unanipenda (1978)* ya J.Simbamwene. Aidha, riwaya ya ujasusi ni riwaya inayohusu upelelezi wa kimataifa. Majasusi ni wapelelezi wanaotumwa na nchi, serikali au waajiri wao kwenda katika nchi nyingine kuchunguza siri zao hasa siri za kijeshi, kiuchumi na kisayansi ili taarifa hizo ziwanufaishe wale waliotumwa. Mfano riwaya ya *The thirty nine steps (1915) ya* J. Buchan na *Mzimu wa Watu wa Kale (1958)* ya M.S Abdulla.

Riwaya changamanini aina nyingine ya riwaya ambayo ina muundo mgumu na inayohitaji umakini kuielewa. Kwa kawaida msuko wa riwaya hii huwa tata. Inawezekana pakawepo na matumizi mapana ya mbinu rejeshi, upana mkubwa wa wahusika na mandhari na matumizi mengi ya lugha ya kitamathali. Mfano riwaya ya *Mzingile (1991)* ya E. Kezilahabi. Vilevile, riwaya sahilini dhana inayotumiwa kuelezea aina za riwaya ambazo zina muundo rahisi na zinaweza kueleweka kwa urahisi. Kwa mfano riwaya ya *Kaburi Bila Msalaba (1969) ya* P. Kureithi.Riwaya nyingine ni riwaya tatizoambayo inajishughulisha na tatizo au mgogoro fulani katika jamii. Huweza pia kuelezea aina ya riwaya ambayo inachunguza tasnifu au suala fulani la kisaikolojia.

Mfano riwaya ya *Kuli* (1983) ya S. Shafi na *Mafuta* (1995) ya K. Mkangi. Halikadhalika, riwaya ya kidastopia husawiri jamii isiyokuwa ya kawaida na isiyokuako kwa wakati maalumu bali inafikirika tu. Katika jamii hiyo sheria za kawaida za kijamii zimebadilishwa kwa namna inayowafanya watu wengi waishie kutaabika na kuteseka sana. Mfano wa riwaya hizi ni kama vile *Kusadikika (1952) ya* S. Robert na *Walenesi (1995) ya* K. Mkangi. Aidha, riwaya ya kimonolojia ni riwaya ambayo sauti inayotawala ni moja ambayo ni ya mwandishi. Wahusika wanaopatikana katika riwaya hii hudhibitiwa kwa kiasi kikubwa na sauti ya mwandishi. Mfano riwaya ya *Walenesi* na *Mafuta (1995) ya* K. Mkangi.

Riwaya nyingine ni riwaya ya kipolifoni ambayo inahusishwa na urejeleaji ambapo kila wahusika wanapozungumza au kuongea sauti zao mbalimbali zinawakilisha mikabala mbalimbali ya kiitikadi. Mfano riwaya ya *Dunia Mti Mkavu (1980)* ya S. A. Mohamed. Vilevile kuna riwaya ya kitarihi inayojihusisha na mawanda makubwa ya kiwakati na kimandhari. Wahusika wengi walioteuliwa kuakisi hali mbalimbali za kijamii na kiuchumi za wakati maalumu. Mfano riwaya ya *Habari za Wakilindi (1972) ya* A. Hemedi. Sambamba na riwaya hizo tulizokwisha kuzitaja hapo juu pia kuna riwaya ya kisasa niambayo inahusu wanasiasa na maisha yao. Riwaya hizo hudhamiria kuyafichua mambo yanayotendeka kinyume na picha inayoonekana waziwazi. Mfano riwaya ya *Nyota ya Huzuni* (1981) ya G.Liwenga na*Njozi Iliyopotea (1980) ya* C. Mung'ong'o.

Riwaya ya Kitasnifu ni aina nyingine ya riwaya inayojihusisha na tatizo fulani la kijamii hasa kwa nia ya kuwahusisha wasomaji. Mfano riwaya ya *Njozi Iliyopotea (1980) ya*

M.Mng'ong'o na *Nyota ya Huzuni* (1981) ya G.Liwenga. Aidha, riwaya ya kiutopia ni riwaya ambayo inasawiri jamii anayoiona mwandishi kama jamii kielelezo na aghalabu huhusisha sifa za Kifantasia au kinjozi. Mfano wa riwaya hii ni kama *Siku ya Watenzi Wote* (1968) ya S. Robert. Sanjari na aina hizo za riwaya pia kuna riwaya ya kiurejelevu inayorejelea aghalabu katika usimulizi wake. Riwaya ya aina hii huishia kutoa maoni kuhusu usimulizi wake na njia za kubuni na kutunga riwaya ambapo hufichua mbinu zake za kiutunzi. Mfano riwaya ya *Musaleo (2004) ya* K.W.Wamitila. Halikadhalika kuna riwaya ya utetezi ambayo inaeleza matatizo ya kijamii, kiuchumi pamoja na dhuluma inayowapata wanyonge au wasiokuwa na uwezo katika jamii fulani. Hivyo riwaya hii hukusudia kurekebisha hali iliyopo katika jamii. Mfano riwaya ya *Walenisi* na *Mafuta* (1995) ya K. Mkangi; *Vuta n'kuvute* (1983) yaS. A.Shafi. Sanjari na aina hizo za riwaya vilevile kuna riwaya ya chuku ambayo hueleza vituko na masahibu yasiyo kuwa ya kawaida. Riwaya ambayo haizingatii uhalisia na mara nyingi masahibu yake huambatana na mapenzi. Mfano riwaya ya *Alfu lela Ulela* (1928) ya E. Brenn na *Kusadikika* (1951) ya S.Robert.

Aina nyingine ya riwaya ni riwaya ya kinganoni riwaya yenye umbo na mtindo wa ngano mathalani huweza kuwa na wahusika wanyama, visa vyenye kutendeka nje ya wakati wa kihistoria. Mfano riwaya ya *Lila na Fila* (1966) ya J. Kiimbila na *Adili na Nduguze* (1952) ya S. Robert. Pia, riwaya istiara ni riwaya ya mafumbo ambayo umbo lake la nje ni ishara au kiwakilishi tu cha jambo jingine. Mfano riwaya ya *Kusadikika* (1951) ya S.Robert. Aidha, riwaya tendi ni riwaya yenye mawanda mapana kama tendi aghalabu riwaya hii husawili matendo ya ushujaa na masuala mazito ya kijamii yenye kuathiri

historia ya taifa husika. Mfano riwaya ya *Vita na Amani* (1863) ya L. Tolstoi. Mbali na riwaya hizo, vilevile kuna riwaya ya kisayansi ni riwaya inayotumia taaluma ya sayansi kama msingi wa matukio, masahibu na maudhui. Riwaya ya kisayansi hubashiri namna sayansi itakavyo athiri maendeleo ya mwanadamu katika karne zijazo. Mfano riwaya ya *Safari hadi kwenye Kiini cha Dunia* (1864) ya J. Vernes. Riwaya ya kimaadili ni riwaya ambayo ina nia ya kufundisha maadili fulani katika jamii. Mfano riwaya ya *Kufikirika* (1967) ya S. Robert. Pia kuna riwaya ya kimapinduzi ni riwaya ambayo inajadili migogoro na maisha ya binadamu kwa kutafakari kwa mantiki na kina kuhusu mambo ambayo urazini wake hauonekani kwa urahisi. Mfano riwaya ya *Kichwa Maji* (1974) ya Euphrase Kezilahabi.

Hivyo uainishaji wa aina za riwaya kama zilivyojadiliwa na Madumulla, Mulokozi na Wamitila unaweza kuwekwa katika aina mbili kuu za riwaya ambazo ni riwaya ya dhati na riwaya pendwa. Riwaya pendwa ni riwaya ambazo hutungwa kwa lengo la kuburudisha na kumstarehesha msomaji mfano, riwaya za kimapenzi, kimahaba, kiuhalifu, kiupelelezi na kijasusi. Wakati riwaya ya dhati ni riwaya ambazo huchimbua na kuchambua masuala mbalimbali ya kijamii, yaani hutafuta chanzo chake sababu zake mpaka kikatokea athari na suluhisho lake mfano mwandishi wa riwaya ya *Rosa Mistika* amemtumia mhusika Rosa kuonesha tangu alipokuwa mdogo, alipopata elimu ya sekondari, mikasa ya kimaisha aliyopitia hadi suluhisho la mikasa hiyo ambalo ni kujiua. Hivyo tunaweza kusema kuwa aina za riwaya ambazo hukosekana katika kundi la riwaya pendwa zipo katika kundi la riwaya ya dhati.

### 2.2.2 Uainishaji wa Riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka*

Madumulla (2009) ameibainisha riwaya ya *Rosa Mistika* kuwa katika kundi la riwaya ya Kisaikolojia. Riwaya ya kisaikolojia ni riwaya ambayo inaweka mkazo juu ya mikinzano ya ndani ya binadamu, kinafsia, kiakili na kijinsia. Kwa kumtumia mhusika Rosa katika riwaya ya *Rosa Mistika* alikuwa na mikinzano ndani ya nafsi yake iliyomfanya hadi kuchukua uamuzi wa kujiua.

Mulokozi (1996) ameiweka riwaya ya *Rosa Mistik*a katika kundi la visasili kwa maana ya kuwa ni riwaya inayojadili asili, maana na hatima ya maisha ya mwanadamu. Aidha Mulokozi anaendelea kusema kuwa riwaya ya *Gamba la Nyoka* iko katika kundi la sira. Sira ni masimulizi ya kweli kuhusu maisha ya mtu au watu. Sira huweza kuwa wasifu yaani zinazohusu habari za maisha ya mtu zikisimuliwa na mtu mwingine au zaweza kuwa tawasifu yaani habari za maisha ya mtu zikisimuliwa na yeye mwenyewe. Sira iliathiri kuchipuka kwa riwaya hasa kwa kuonesha masimulizi ya maisha ya mtu toka utotoni mpaka uzeeni. Mifano ya hadithi hizi ni; *Kurwa na Doto(1960) ya* (M.S.Farsy), *Rosa Mistika(1971)* na *Gamba la Nyoka(1979) za* (Euphrase Kezilahabi) na riwaya ya *Maisha Yangu na baada ya Miaka Hamsini* (1951) ya (S. Robert).

Hivyo basi, riwaya ya *Rosa Mistika* inaingia katika kundi la riwaya za Kisaikolojia kwani kwa kiasi kikubwa riwaya hii imezungumzia mikinzano iliyoko ndani ya nafsi ya mtu, ingawaje si rahisi riwaya kuegemea katika kundi moja pekee, lakini kinachopaswa kutazamwa ni jinsi gani maudhui yaliyopo yameegemea katika aina gani ya riwaya.

Hivyo, ninakubaliana na Madumulla (2009) kuwa riwaya ya *Rosa Mistika* imeegemea katika kundi la riwaya ya Kisaikolojia. Aidha, sipingani na Mulokozi (1996) pale anapoiweka riwaya ya *Rosa Mistika* katika kundi la visasili kwani imeelezea asili ya mhusika Rosa tangu kuzaliwa hadi kifo chake. Halikadhalika, sikubaliani na mawazo ya Mulokozi (1996) kuiweka riwaya ya *Gamba la Nyoka* katika kundi la sira kwa sababu riwaya hii haielezei maisha ya mtu tangu kuzaliwa hadi kufa bali riwaya hii ya *Gamba la Nyoka* inafaa kuingia katika kundi la riwaya ya kihistoria kutokana na kuzungumzia historia ya Tanzania katika kipindi cha Azimio la Arusha katika ujenzi wa vijiji vya ujamaa.

**2.3 Tafiti Zinazohusiana na Riwaya za Euphrase Kezilahabi**

Senkoro (1976) anazungumzia riwaya ya *Rosa Mistika* iliyoandikwa na Euphrase Kezilahabikuwa ni riwaya inayoangalia migongano ya kitamaduni, kiuchumi na kisiasa katika jamii na kuhusianisha na unafsia. Uhusiano kati ya utamaduni wa asili na njia mpya za maisha ya nyakati hizi za leo unafanya huo utamaduni uwe kiini cha mabishano yanayoletwa na kutopatana kati ya muundo mpya wa uchumi na maisha ya jamii. Senkoro anahitimisha kwamba riwaya ya *Rosa Mistika* imeonesha migongano ya aina hiyo hasa kinafsia.Andiko la Senkoro ni muhimu katika utafiti wetu kwani limetusaidia kujua maudhui mbalimbali yabebwayo katika riwaya ya *Rosa Mistika*na kwa kupitia maudhui hayo ndipo hapo tutaona matumizi ya maneno na sentensi mbalimbali katika kuwasilisha ujumbe wake ikiwemo matumizi ya maneno ya Biblia. Hivyo basi, utafiti

huu umejikita kuangalia utumizi wa maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka*na si maudhui kama ilivyojitokeza katika utafiti wa Senkoro.

Mosha (2013) alifanya utafiti kuhusu usawiri wa mhusika Padri katika riwaya za Euphrase Kezilahabi ambazo ni*Rosa Mistika, Gamba la Nyoka* na *Nagona*. Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kwamba mhusika Padri anasawiriwa katika nafasi mbalimbali kama vile kiongozi wa kanisa katika jamii, mwanaume wa kawaida katika jamii ambapo anaonekana katika matendo kama vile uzinzi na ulevi pamoja na mtu mwenye sauti katika jamii. Vilevile, mhusika Padri anawasilisha dhamira kuu nne ambazo ni suala la malezi ya kiroho, unafiki wa viongozi wa kanisa Katoliki, uonevu na kukosekana haki na suala la uwezo wa Padri kuondoa dhambi. Utafiti wa Mosha umesaidia utafiti huu kuonesha picha halisi ya nafasi ya Padri kama kiongozi wa dini katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka*. Mhusika Padri katika kutekeleza wajibu wake ametumia maneno mbalimbali ya kimungu ambayo mengine yamo katika Biblia na ndio hasa kiini cha utafiti huu.

Mfinanga (2017) alifanya utafiti kuhusu ujinabishaji wa motifu ya kifo katika riwaya ya *Rosa Mistika, Kichwa Maji, Gamba la Nyoka* na *Dunia Uwanja wa Fujo* za Euphrase Kezilahabi. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya wanaurasimu wa Kirusi.Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kuwa hakuna matini ya kifasihi inayoandikwa bila kukengeushwa huko ndiko kunakoleta ujumi wa kazi husika za kifasihi na upekee wenye kuvuta makini ya wasomaji.  Aidha matumizi ya mbinu ya uajinabishaji, ishara na chuku katika riwaya

ya *Rosa Mistika, Kichwa Maji, Gamba la Nyoka* na *Dunia Uwanja wa Fujo* imebainika kuwa huweza kumfanya msomaji alione tukio au jambo alilolizoea kama vile anakutana nalo kwa mara ya kwanza.Andiko hili limetusaidia katika utafiti huu kwa sababu katika kubaini uanajibishaji wa motifu ya kifo katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka* mwandishi ametumia maneno ya Biblia katika kufikisha ujumbe ambapo utafiti huu unashughulika nayo.

Makhino (2017) alifanya utafiti kuhusu ukanushi-udhanaishi wa Rosa katika riwaya ya *Rosa Mistika* ya Euphrase Kezilahabi. Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya ukanushi-udhanaishi. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha ukanushi wa mhusika mkuu ambaye ni Rosa katika riwaya teule jinsi ulivyosawiriwa na dhamira zake katika fasihi. Dhamira hizo ni maafa, usaliti, ubwege na mapenzi. Andiko hii limesaidia utafiti huu kuona jinsi tabia ya mhusika Rosa kama vile usaliti, umalaya, ilivyomfanya mwandishi kutumia maneno ya Biblia, katika kufikisha ujumbe katika jamii. Sambamba na hilo tumeona jinsi mwandishi alivyomtumia mhusika Rosa kama mhusika mdhanaishi kwa kumuonesha jinsi alivyokata tamaa ya maisha hadi kufikia hatua ya kujiua. Katika kumfafanua mhusika Rosa, matumizi mbalimbali ya maneno ya Biblia yametumika ambayo ni kiini cha utafiti huu.

## 2.4 Dhana ya Dini

Omari na Mvungi (1981) kwa upande waowanaitazama dini kama mfumo wa kiitikadi, viashirisho na matendo, mambo na vitu ambavyo hueleweka na kutambulika kwa njia ya imani na si kwa njia ya utafiti wa kitaaluma. Zaidi, wanaona kuwa dini ni lazima imhusishe mwanadamu na Mungu au viumbe vingine viishivyo ambavyo huaminika kuwa vinayo mamlaka makubwa kuliko mwanadamu. Wanaoamini Mungu huwa na imani kuwa, kuna maisha baada ya kufa au maisha ya ulimwengu ujao ambayo hayafahamiki kitaaluma, kiutafiti au kutawaliwa nayo.

Malugu (2015) anadai kuwa hapo zamani nyenzo iliyokuwa ikitegemewa sana ilikuwa ni dini. Dini ilimsaidia mwanadamu kutambua kuwa vitu vyote vilivyopo duniani kama vile mito, radi, mvua, ndege, wanyama, samaki na pia yeye mwenyewe ilitokana na nini au vilitoka wapi. Malugu (ktj) anaendelea kusema kuwa mafunzo ya dini yalisaidia kuondoa migogoro mingi iliyokuwepo kama vilemapigano, vita na watu kuuana. Kwa hiyo, dini ilikuwa na nafasi ya kuwaunganisha watu katika jamii moja au jamii mbalimbali. Aidha, Malugu anaitazama dini kama kitu cha mtu binafsi, kitu ambacho ni cha itikadi na imani.Vilevile, anahitimisha kwa kusema kuwa, madhumuni ya dini ni kumfanya mwanadamu aishi vema hapa duniani ili baada ya kifo aingie peponi huko ahera.

Kutokana na maelezo ya wataalamu hao, hapana shaka kuwa dini ni chombo cha kiitikadi au kiimani ambacho kinafungamanishwa na imani ya kuwepo pepo au mbingu; mahali ambapo huaminika kuwa ni watenda mema tu ndio watakaostahili kuingia. Vile vile, dini inaonekana kuwa na nafasi muhimu sana katika jamii yoyote.

Tanzania ni moja ya nchi katika Afrika Mashariki inayokadiriwa kuwa na idadi ya watu milioni 44.9 (National Bureau of Statistics, 2012). Pembe (Ht) anaeleza kuwaTanzania ina makundi mawili makubwa ya dini ambayo ni Wakristo na Waislamu. Pembe anaendelea kueleza kwamba, pamoja na kuwepo kwa makundi mawili makubwa ya dini ambayo ni Ukristo na Uislamu lakini wapo vilevile wanaoamini dini za asili, pamoja na Kihindi. Dini hizi hutofautiana katika namna ya kuabudu, ukaaji ndani ya ibada na mtume wanayepitia kumwabudu japokuwa wote huamini yupo Mungu anayeishi. Kwa mfano Waislamu humwamini Mungu kupitia Mohammed ilhali Wakristo humwamini Mungu kupitia Yesu Kristo. Katika suala la ukaaji ndani ya ibada, Waislamu hawachangamani baina ya wanawake na wanaume wakati imani ya Kikristo wao wanaume na wanawake wanakaa pamoja hata ndani ya benchi moja.

## 2.5 Tafiti Zihusuzo Dini

Marisya (2017) alifanya utafiti kuhusu mchango wa sajili ya kidini katika kufanikisha riwaya mbili za Ken Walibora *Kidagaa Kimemwozea*na *Ndoto ya Almasi*. Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya pragmatiki leksika. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa sifa za sajili ya dini ya Kikristo zinadhihirika katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*na*Ndoto ya Almasi.* Baadhi ya sifa hizo ni kama vile msamiati unaosifu

Mungu,matumizi ya mafumbo na nyimbo za kumsifu Mungu. Pia utafiti huu ulidhihirisha kuwa sajili ya dini ya Kikristo imemwezesha mwandishi wariwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*na *Ndoto ya Almasi*kufanikiwa katika kujenga maudhui,dhamira na wahusika. Utafiti wa Marisya (Ktj) umesaidia utafiti huu kubaini namna watafiti wengine walivyochambua riwaya nyingine zilizotumia maneno ya Mungu japokuwa utafiti wa Marisya (Ktj) haujajikita moja kwa moja katika kuchunguza maneno ya Biblia kama ambavyo utafiti huu unachunguza. Sanjali na hilo, pia imeonesha kuwa si mwandishi Euphrase Kezilahabi tu anayetumia maneno kutoka katika vitabu vya dini bali wapo waandishi wengine pia waliotumia sajili ya dini katika kufikisha ujumbe katika jamii.

Msangi (2018) alifanya utafiti kuhusu kuchunguza Ubiblia katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo kupitia tamthiliya zake za *Nyerere na Safari ya Kaanani (2015) na Sadaka ya John Okello (2015)*. Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya mwingiliano matini. Matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwa kuna Ubiblia mwingi katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo alizoandika miaka ya hivi karibuni. Vipengele vya kifani ndivyo vilivyotumika katika kubainisha Ubiblia huo ambavyo ni jina la kitabu, hadithi za Biblia, wahusika wa Biblia, nukuu za Biblia na mtindo wa ushairi. Sababu za matumizi ya maneno hayo ni matokeo na athari ya mafundisho na mapokeo ya Ukristo ambayo yalimuathiri mtunzi na kuyatumia mapokeo hayo kuzalisha tamthiliya hizo. Tofauti ya utafiti wa Msangi na utafiti huu ni kwamba Msangi amechunguza Ubiblia katika tamthiliya*,* wakati utafiti huu umejikita katika kuchunguza matumizi na athari za maneno ya Biblia katika riwaya.

Pembe (Ht) ameandika makala kuhusu majina ya Wakristo nchini Tanzania. Makala hiyo iliongozwa na nadharia sababishi. Makala imebaini kwamba majina mengi ya Wakristo nchini Tanzania yana asili ya nchi za Kimagharibi ambako dini ya Kikristo ilianzia. Aidha makala imegundua kuwa majina ya Kikristo yanatokana na majina ya Mungu, nabii, mitume, watakatifu na majira ya dini. Sambamba na ugunduzi huo, makala imebaini kuwa wale wanaopewa majina ya urithi hawaishi kulingana na tabia za mhusika halisi wa jina. Hii ina maana kwamba tabia ya mhusika anayerithi jina inakuwa tofauti na tabia ya mwanzilishi wa jina na hivyo kupoteza maana halisi ya jina husika. Makala haya yametusaidia kujua historia ya dini nchini Tanzania pamoja na mgawanyiko wa makundi ya madhehebu yaliyoko nchini Tanzania. Sambamba na hilo, makala imedhihirisha kuwa hata kazi za fasihi ikiwemo riwaya huakisi hali halisi ya jamii ikiwemo matumizi ya maneno ya Biblia.

## 2.6 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya uhemenitiki.Uhemenitiki ni nadharia inayohusiana na uelewaji na kutafsiri matini. Chimbuko la nadharia hii ni katika uchambuzi wa falsafa katika matini za kidini, hususani dini ya Kikristo. Waasisi wanaohusishwa na chimbuko la nadharia hii ni kama vile Friedrich Schleiermacher (1768-1834), Wilhem Dilthey (1833-1911) na Martin Heidegger (1889-1976).Akizungumzia suala la mviringo au duara la Kihemenitiki, Senkoro (1989:9) anasema:

> …katika usomaji kuna mviringo wa kihemenitiki ambao
> humfanya msomaji aende mbele na nyuma, kushoto na kulia

> mwa yale yaongelewayo katika kaziya fasihi. Hadhira huwa wanabashiri na kuhusisha mambo wanayoyapitia maishani mwao.

Msingi mkubwa wa nadharia ya uhemenitiki ni imani ya kwamba matendo ya binadamu yanaathiriwa kwa njia mbalimbali na asasi tofauti zilizoko katika mazingira yake. Msingi huo unatupeleka katika dhana ya kuibua umuhimu wa kuelewa njia au mbinu za uelewaji wa maana za matini. Madai ya msingi wa nadharia ya uhemenitiki yanahusisha dhana mbalimbali kama vile duara la kihemenitiki, utukuzaji pamoja na ile ya ufufuaji wa kisarufi, kisaikolojia na kimuktadha (Ponera, 2010).

Kulingana na nadharia hii ya uhemenitiki huwa kuna ugumu wa kuwepo kwa uwiano kati ya malengo na maana asilia ya mtunzi dhidi ya uelewaji wa maana aipatayo msomaji. Uelewaji wa maana kwa msomaji huhusisha kuyajua mambo mbalimbali yaliyomzunguka mtunzi wakati au kabla ya kuitunga kazi husika. Kwa kufanya hivyo, ndipo msomaji atakuwa amelitalii duara la kihemenitiki (Ponera, 2010).

Dhana ya utukuzaji katika nadharia ya uhemenitiki inamaanisha jumla ya makisio mbalimbali ambayo msomaji au mhakiki wa kazi ya fasihi huwa nayo punde aishikapo kazi yoyote ya kifasihi. Makisio hayo hujengwa akilini mwa msomaji kulingana na misingi mbalimbali kama vile anwani yake (jina na picha ya kitabu), kiwango cha usomi, utamaduni, upeo wa uelewa, pamoja na ulinganisho wa kazi zozote zilizotungwa na watunzi wengine zinazofanana na hiyo (Wamitila, 2002).

Wamitila (2002) anafafanua kuwa dhana ya ufufuaji, hususani ule wa kisaikolojia iliasisiwa na Dilthey (1833-1911). Wamitila anaeleza kuwa, kuna umuhimu mkubwa kwa msomaji au mhakiki kufufua muktadha asilia wa kazi inayohusika na kujaribu kujiweka katika muktadha huo ili aweze kuipata maana asilia ya matini. Kwa mujibu wa mawazo yake, kazi mbalimbali za kifasihi zinaweza kuwa na maana mbalimbali kwa wasomaji mbalimbali. Aidha, dhana ya ufufuaji inasisitiza kuwa ili kuielewa na kuitafsiri maana ya matini lazima msomaji au mhakiki azame katika kuuelewa mtindo. Hapa neno 'mtindo' limetumika kumaanisha muktadha wote wa mfumo wa maneno na sentensi zilizotumika katika matini.

Dhana hizi zinazobeba madai ya msingi ya nadharia ya uhemenitiki zinahusiana kwa kiasi kikubwa. Gadamer (1960) ambaye amenukuliwa na Senkoro, (1987:7) anasema, taaluma ya uhemenitiki hujihusisha na utafutaji wa maana ya kazi ya fasihi kwa kuuliza maswali muhimu manne ambayo ni:

i. Nini maana ya fasihi?

ii. Je, maana hii inahusianaje na kusudi la mwandishi?

iii. Je, tunaweza kuzielewa kazi za fasihi za tamaduni na historia tofauti na zetu?

iv. Je, ni rahisi kupata uelewaji wa ndani wa kazi ya fasihi au huu hutegemea mazingira na historia ya hadhira ihusikayo.

Katika kujibu maswali haya, ndipo tunapohusisha misingi ya nadharia hii. Kulingana na malengo ya utafiti huu nadharia ya uhemenitiki inafaa zaidi katika kufikia malengo yaliyokusudiwa. Katika utafiti huu nadharia ya uhemenitiki imetumika kuchunguza na kubainisha matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka* kutokana na kuona kuwa misingi yake ilihusiana sana na malengo ya utafiti huu. Misingi hiyo ambayo ni imani na utukuzaji, imeongoza katika kubainisha matumizi ya maneno ya Biblia, dhima na athari zake kwa Wakristo. Msingi wa kwanza ambao ni imaniunaeleza kwamba matendo ya binadamu huathiriwa na asasi mbalimbali zilizomo katika mazingira yake. Halikadhalika msingi wa utukuzaji unaeleza kwamba jumla ya makisio mbalimbali ambayo msomaji au mhakiki wa kazi ya fasihi huwa nayo punde aishikapo kazi yoyote ya kifasihi. Makisio hayo hujengwa akilini mwa msomaji kulingana na misingi mbalimbali kama vile kiwango cha usomi, utamaduni, na upeo wa uelewa. Hivyo, misingi miwili ambayo ni imani pamoja na utukuzaji imetumika katika uchambuzi na ufafanuzi wa data.

## 2.7 Pengo la Utafiti

Baada ya kutalii kazi za tafiti mbalimbali ambazo zimeeleza kuhusu suala la uandishi wa Euphrase Kezilahabi katika kazi mbalimbali za fasihi, utafiti huu umebaini kuwa tafiti nyingi zilizofanywa zimejikita katika kuchunguza masuala mengine kama vile tabia za ukanushi-udhanaishi wa Rosa katika riwaya ya *Rosa Mistika* kama vile kujiua, kukata tamaa ya maisha, ujinabishaji wa motifu ya kifo katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka* na usawiri wa mhusika Padri katika riwaya ya *Rosa Mistika*, *Gamba la*

*Nyoka*na *Nagona* lakini hazijagusia suala la utumizi wa maneno ya Biblia. Hivyo tumeona ni vema kushughulikia kipengele cha matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya zake teule ili kuziba pengo la kitaaluma lililoachwa wazi na wanazuoni mbalimbali waliotangulia.

**2.8 Hitimisho**

Sura hii imeelezea mapitio mbalimbali ya tafiti zilizotangulia ikiwemo dhana ya riwaya, dini, historia ya mwandishi wa riwaya teule pamoja na muhtasari wa riwaya teule. Aidha, pengo la utafiti limebainishwa na ndilo lililomsukuma mtafiti kufanya utafiti huu. Vilevile, kiunzi cha nadharia kilichoongoza utafiti huu kimefafanuliwa. Sura inayofuata inahusu mbinu za utafiti zilizotumiwa katika utafiti huu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Sura hii inahusu mbinu na njia mbalimbali zilizotumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data. Mbinu za utafiti ni mambo yanayofanywa na mtafiti kwa kuongozwa na kiunzi cha nadharia ili kufikia malengo ya utafiti (Jonker na Pennink, 2010). Sura hii imehusisha vipengele mbalimbali kama vile muundo wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, na mbinu za ukusanyaji data. Aidha, sura hii imefafanua zana za utafiti, uchambuzi wa data pamoja na uthabiti, kuaminika na maadili ya utafiti.

## 3.1Muundo waUtafiti

Muundo wa utafiti hutoa picha kamili inayoonesha namna utafiti ulivyofanyika tangu kukusanya data mpaka kuchambua data za utafiti (Kothari, 2008). Watafiti wengine huita muundo wa utafiti kuwa ni usanifu wa utafiti ambao hutoa ramani kamili ya utafiti mzima vile ulivyofanyika katika kila hatua. Utafiti huu umefanyika kwa kuzingatia muundo wa uchunguzi kifani ambapo riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka* zimeteuliwa na kutafitiwa ili kuwezesha kupata data za msingi za utafiti huu. Uchunguzi kifani ni muundo wa utafiti ambapo mtafiti huteua eneo au kitu maalum ambacho kitashughulikiwa na kuwezesha kupatikana kwa data za utafiti zilizokusudiwa. Uchunguzi kifani ni mbinu nzuri ya kumwezesha mtafiti kupata data anazohitaji (Cresswell, 2009).

## 3.2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni mahali ambapo mtafiti amechagua kwa lengo la kupata data za kujibu maswali ya utafiti (Creswell, 2009). Eneo la utafiti huteuliwa kutokana na lengo kuu la utafiti ili kuwezesha kupata data toshelevu na sahihi zitakazokidhi malengo mahususi ya utafiti. Kwa kuzingatia maelezo hayo, eneo la utafiti huu ni riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka*. Eneo la utafiti limechaguliwa kwa sababu mwandishi ametumia maneno ya Biblia zaidi katika riwaya hizo, hivyo zimewezesha kupata data zilizojibu maswali ya utafiti huu.

## 3.3 Sampuli

Sampuli ni kundi fulani la watu lililomo ndani ya mkusanyiko wa watu ambao mtafiti anaamini kwamba linazo habari zitakazomwezesha kujibu swali lake la utafiti (Mligo, 2012). Sampuli ya utafiti huu ni riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka.* Mtafiti ameteua riwaya hizo kwa sababu zimeonesha kutumia maneno ya Bibliakwa kiwango kikubwa hivyo kuweza kutimiza malengo ya utafiti.

### 3.3.1Usampulishaji

Usampulishaji ni kitendo cha kuchagua sampuli kutoka kundi lengwa yaani kuchagua washiriki kutoka katika kundi kubwa la dhana, vitu na watu ili kutoa jumuisho litakalojumuisha sifa za kundi husika (Kothari, 2004). Usampulishaji hutegemea taarifa, muda na fedha zilizotengwa kwa ajili ya utafiti.Katika utafiti huu,

Usampulishajilengwaulitumika katika mchakato wa upatikanaji wa data za utafiti. Ranganatham na Krishnaswami (2010) wanaeleza kwamba sampuli lengwa ni sehemu ndogo ya jamii au kitu fulani au vitabu ambavyo mtafiti huchagua ili utumike katika utafiti kwa sababu tu ya kuwa na sifa za kukidhi mahitaji ya utafiti huo. Uteuzi wasampuli lengwa unatokana na kwamba katika mbinu hii mtafiti hulenga kundi fulani la watu, vitu, au dhana zinazoaminika kuwa na uhakika juu ya utafiti husika (Tromp na Kombo, 2006).

Usampulishaji lengwa umetumika katika uteuzi wa riwaya pamoja na uteuzi wa matini zilizotumika katika uchambuzi. Uteuzi wa riwaya ulijitokeza pale ambapo mtafiti aliposoma kwa makini riwaya mbalimbali na kubainisha makundi mawili ya riwaya ambayo ni riwaya zilizotumia maneno ya Biblia na kundi la pili ni riwaya ambazo hazikutumia maneno ya Biblia. Mtafiti alichukua kundi la riwaya zilizotumia maneno ya Biblia ambazo zilikuwa tano na kuzisoma tena kwa makini huku akiorodhesha idadi ya maneno ya Biblia yaliyotumika. Katika kufanya mchakato huo, mtafiti alibaini riwaya mbili ambazo ni *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka* zimetumia maneno mengi ya kwenye Biblia kuliko riwaya nyingine na hivyo kuziteua kuwa sampuli ya utafiti huu. Mtafiti alizisoma kwa umakini tena riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka* na kubaini maneno yote yaliyotumia Ubiblia na kuwa matini ya data za utafiti huu. Hivyo utafiti huu umetumia sampuli lengwa kuchagua riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba laNyoka* kwa kuwa zimeonesha kuwa na kiwango kikubwa cha maneno ya Biblia yaliyowezesha kupata data za kutosha kukamilisha malengo ya utafiti huu.

### 3.4 Mbinu za Ukusanyaji Data

Mbinu za ukusanyaji data ni njia mbalimbali anazozitumia mtafiti katika kukusanya data ili kupata taarifa zinazotakiwa (Nsebemuki, 2004). Kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu, mtafiti ametumia mbinu ya upekuzi matini. Upekuzi matini ni mbinu inayojumuisha usomaji wa matini mbalimbali kama vile vitabu, majarida, magazeti, pamoja na matini za mazungumzo ambazo hazijaandikwa (Kothari 2009). Katika utafiti huu upekuzi matini ulitumika kusoma riwaya teule kwa makini na mara nyingi ili kupata data zilizokusudiwa. Katika kufanikisha mchakato huu, utafiti umezingatia utaratibu maalumu kwa hatua tatu ambazo ni: Kwanza mtafiti aliweka bayana mambo ambayo anakusudia kuyapata kutoka katika matini alizoziteua ili kutimiza malengo ya utafiti. Pili, mtafiti alisoma matini husika kwa makini ili aelewe vizuri. Tatu mtafiti alianza kukusanya data kwa kunukuu katika daftari maalumu aliloandaa kwa ajili ya nukuu data ambazo ndizo data za msingi za utafiti zenye kujibu maswali ya utafiti.

Mbinu hii inafaa katika utafiti huu kutokana na ukweli kuwa, utafiti umejikita katika matini zilizoandishi. Mbinu ya upekuzi matini humsaidia mtafiti kupata data ambazo ni za uhakika kutokana na uhifadhi wake pamoja na kumsaidia mtafiti kuwa na uwezo wa kurudia kuziangalia data zake kwa urahisi ili kupata uhakika zaidi wa data zenyewe (Denscombe, 1998).

Katika utafiti huu, mtafiti alipekua riwaya teule zenye maneno ya Biblia zilizopatikana kutokana na sampuli lengwa. Mtafiti alizisoma riwaya teule mara kadhaa huku akinakili maneno yote yenye Ubiblia. Baada ya kunakili maneno hayo katika riwaya teule zote, mtafiti alianza kupitia unukuzi wa matini zake moja baada ya nyingine huku akiziainisha na kuzipanga katika ruwaza zake matini ambazo zinajibu malengo ya utafiti kwa ajili ya uchambuzi. Baada ya kuziweka matini kiruwaza, mtafiti alitumia mbinu ya usampulishaji lengwa kuchagua matini husika ambazo zimetumika katika uchambuzi wa data. Matini zilizochaguliwa katika uchambuzi zimeweza kutoa taarifa ya dhima na athari za utumizi wa maneno ya Biblia kwa kurejelea riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka* Sambamba na riwaya hizo utafiti uliweza kupata data pia kwenye tafiti mbalimbali, makala, machapisho yanayohusiana na mada ya utafiti wake ambapo uliweza kujua maana ya matumizi ya maneno ya Biblia kama yalivyojitokeza katika riwaya teule.

### 3.5 Zana za Utafiti

Zana za utafiti ni vitu ambavyo mtafiti huvitumia katika ukusanyaji wa data (Kothari, 2009). Katika kufanikisha utafiti, mtafiti ametumia zana mbalimbali katika kukusanya data na kuandika kazi hii ya utafiti kutokana na mazingira yake husika. Vifaa lengwa hasa vilivyotumika ni kalamu na shajara, ngamizi, kihifadhi data nje na kinyonyi.

#### 3.5.1 Kalamu na Shajara

Mtafiti ametumia kalamu na shajara maktabani kunukuu dondoo muhimu wakati wote alipokusanya data za awali na za upili katika riwaya teule, tasnifu tangulizi, majarida,

machapisho na vitabu mbalimbali vilivyohusu mada ya utafiti hususani katika kazi za fasihi na kuziandika kwenye shajara kwa kutumia kalamu.

### 3.5.2 Ngamizi

Ngamizi imemsaidia mtafiti kutunza data za maktabani.Pia ngamizi imetumika kama sehemu ya maktaba tembezi au maktaba ya kidijitali kutokana na huduma ya mtandao.Hivyo kifaa hiki kimemsaidia wakati wote wa utafiti kuanzia maandalizi ya awali ya utafiti, wakati wa kutafuta data, kuchanganua data na pia kuandaa na kukamilisha ripoti ya utafiti.

### 3.5.3 Kihifadhi Data Nje

Kihifadhi data nje ni kifaa ambacho mtafiti ametumia kuhifadhia nakala tepe zote kuhusu utafiti ambazo zimo katika ngamizi ili endapo patatokea hitilafu ya ngamizi taarifa za utafiti ziwe salama katika sehemu ya ziada. Kifaa hiki ni muhimu sana katika zoezi zima kwani tangu mwanzo mpaka utafiti ulipokamilika kihifadhi data nje kimetumika kuhifadhi ripoti nzima ya utafiti.

### 3.5.4 Kinyonyi

Mtafiti ametumia kifaa hiki kutunza nakala tepe zinazohusiana na utafiti kama ilivyo ngamizi na kihifadhi data nje.Kifaa hiki ni muhimu sana katika zoezi zima kwani tangu mwanzo mpaka utafiti ulipokamilika kinyonyi kimetumika kuhifadhi ripoti nzima ya utafiti.

### 3.6 Uchambuzi na Uwasilishaji wa Data

Data zinazokusanywa wakati wa utafiti, hazina budi kufanyiwa uchambuzi kwa lengo la kujibu maswali ya utafiti na kukamilisha lengo liliokusudiwa (Babbie, 1999). Uchambuzi wa data ni kitendo cha kufafanua data zilizokusanywa ili ziweze kueleweka na kuleta maana iliyokusudiwa (Frenkel, 1998). Kwa maana hiyo data za utafiti huchambuliwa kwa kutumia mbinu stahiki za kiutafiti ambapo katika utafiti wetu mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo na kitakwimu ndizo zilizotumika.

Katika utafiti huu, mtafiti amekusanya data akiongozwa na maswali ya utafiti na kuziweka data hizo katika makundi makuu matatu. Kundi la kwanza ni kubainisha matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka*. Kundi la pili ni kueleza dhima za matumizi ya maneno ya Biblia na kundi la tatu ni data zilizohusu athari za matumizi ya maneno ya Biblia kwa Wakristo. Baada ya hapo mtafiti amechagua data chache kutoka kila kundi kwa kuongozwa na nadharia ya Uhemenitiki na kuzinukuu kisha kuzitolea ufafanuzi kwa njia ya maelezo kwa sababu mwelekeo wa utafiti huu kwa kiwango kikubwa ni wa kimaelezo hivyo basi, taarifa za kitakwimu zimejitokeza kwa uchache. Kwa mujibu wa Baradyana na Ame (2007) tafiti za kimaelezo hutumia mbinu ya maelezo, ulinganisho, pamoja na uhusishaji wa data dhidi ya nadharia katika kuchanganua data na kutoa matokeo. Utafiti huu umechunguza matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika*na*Gamba la Nyoka* kwa kutumia nadharia ya Uhemenitiki kama mwega wa mwelekeo wa utafiti mzima hususani katika

uchambuzi wa data za msingi.Mtafiti ametoa maelezo ya kina kuhusu dhima za matumizi ya maneno ya Biblia pamoja na athari za maneno hayo kwa Wakristo.

### 3.7 Uthabiti, Kuaminika na Maadili ya Utafiti

Durheim na Wassenaar (2002) wanaeleza kwamba vipengele vya uthabiti, maadili na kuaminika kwa utafiti ni vya muhimu katika aina yoyote ile ya utafiti, ingawa mbinu za utafiti hutegemea aina ya utafiti kama ni wa kimaelezo au wa kitakwimu.

#### 3.7.1 Uthabiti wa Data

Denscombe (1998) anaeleza kuwa utafiti huwa thabiti iwapo data zilizotumiwa katika utafiti zitaonekana kuwa ni sahihi na za kweli. Katika utafiti huu kipengele cha uthabiti wa utafiti kimezingatiwa kwa kutumia mbinu ya upekuzi matini iliyohusisha kusoma riwaya teule na nyaraka mbalimbali zilizowezesha upatikanaji wa data sahihi zilizotimiza malengo ya utafiti.

#### 3.7.2 Kuaminika kwa Utafiti

Bryman (2004) anaeleza kwamba utafiti huwa wa kuaminika ikiwa utafiti huo utarudiwa tena kwa kutumia mbinu zilezile zilizotumiwa katika tafiti za awali na kutoa matokeo yanayofanana au yenye kuonesha uelekeo mmoja. Katika utafiti huu, kipengele cha kuaminikakwa utafiti kimezingatiwa kwa kutoa maelezo kuntu na mifano kutoka katika Biblia katika kujenga hoja zenye kuaminika.

### 3.7.3 Maadili ya Utafiti

Padgett (2004) anabainisha kwamba, masuala ya kimaadili huibuka katika aina zote za utafiti, na utafiti usio wa kitakwimu ukiwemo. Utafiti huu umezingatia vipengele vya maadili hasa katika kuhakikisha kuwa kanuni na taratibu za ufanyikaji wa tafiti zimefuatwa. Kanuni hizo ni kama vile upatikanaji wa vibali vilivyomruhusu mtafiti kuingia maktabani, kuhakikisha kwamba mada ya utafiti inafaida kwa jamii na kuhakikisha kwamba kanuni za uandishi zimefuatwa.

## 3.8 Changamoto za Utafiti

Shughuli yeyote ile haikosi kuwa na changamoto kadha wa kadha. Ndivyo ilivyo pia katika utafiti. Changamoto mojawapo iliyompata mtafiti katika mchakato mzima wa uandishi wa tasnifu hii ni ufinyu wa muda. Mtafiti alikuwa hana budi kufanya utafiti huku akitimiza majukumu ya kazi, hali hii ilimfanya mtafiti kutumia muda mrefu kukamilisha utafiti. Pamoja na changamoto hiyo, mtafiti hakukata tamaa katika kuhakikisha kwamba anatimiza majukumu ya kazi huku akiendelea kuandika utafiti muda wa usiku. Pamoja na kwamba muda wa usiku ulikuwa mdogo lakini utafiti uliweza kukamilika.

## 3.9 Hitimisho

Kimsingi sura hii inahusu mbinu zilizotumika katika zoezi zima la utafiti. Hivyo sura hii imefafanua mbinu kadhaa ambazo ni muundo wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji. Mbinu nyingine zilizofafanuliwa katika sura hii ni mbinu za ukusanyaji data, zana za utafiti, uchambuzi wa data,usahihi, kuaminika na maadili ya utafiti pamoja na changamoto za utafiti. Aidha sura hii imeeleza sababu za kuteua mbinu hizo za utafiti. Sura inayofuata inaeleza uwasilishaji na uchanganuzi wa data.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inawasilisha na kujadili data za utafiti ili kuweza kukamilisha malengo mahususi ya utafiti huu kama tulivyoona katika sura ya kwanza. Data za msingi zimepatikana kwa kutumia riwaya teule za Euphrase Kezilahabi ambazo ni *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka.* Sura hii imegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni kubainisha matumizi ya maneno ya Biblia, dhima za matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya hizo na athari za matumizi ya maneno ya Biblia kwa Wakristo. Hitimisho la sura hii linapatikana katika sehemu ya nne.

## 4.1 Matumizi ya Maneno ya Biblia katika Riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka*

Hili lilikuwa lengo mahususi la kwanza katika utafiti huu ambalo lililenga kubainisha matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka* zilizoandikwa na Euphase Kezilahabi. Ili kuhakikisha lengo hili linatimia mtafiti alisoma riwaya zote mbili mara kadhaa kwa utaratibu na umakini zaidi na kubaini maneno ya Biblia yaliyotumika katika kufikisha ujumbe katika jamii kama vile Kunyweni hii ndio damu yangu, Maskini wa Roho, Picha ya Mtu Msalabani, Kutubu dhambi, Kiti cha Enzi,

Damu Yao na iwe Juu ya Vichwa Vyenu, Mimi Ninanawa Mikono kama Pilato, Baba ikiwezekana Kikombe hiki Kinipite, Kwa Jina la Baba, na Mwana na la Roho Mtakatifu, haleluya, kubatizwa kwa jina la Emanuel, utakatifu, Mungu na Maria, Mama wa Mungu Aliyezaa kwa Nguvu za Roho Mtakatifu.

**Jedwali 4.1: Idadi ya maneno ya Biblia yaliyotumika katika Riwaya ya *Rosa Mistika*na*Gamba la Nyoka***

| Jila la Kitabu | Idadi ya Maneno Ya Biblia | Idadi ya Matini Zilizoteuliwa |
|---|---|---|
| **Rosa Mistika** | 16 | 5 |
| **Gamba la Nyoka** | 12 | 4 |
| **Jumla** | 28 | 9 |

**Chanzo**: Data za Utafiti, (2019)

Jedwali 4.1 hapo juu, linaonesha kwamba riwaya ya *Rosa Mistika*na *Gamba la Nyoka*, zote zimetumia maneno ya Biblia katika kuhakikisha jamii inafikiwa na ujumbe kama alivyokusudia mwandishi wa vitabu hivi. Jedwali linaonesha kwamba, kati ya riwaya zote mbili, riwaya ya *Rosa Mistika* imetumia idadi kubwa ya maneno ya Biblia ukilinganisha na riwaya ya *Gamba la Nyoka.* Aidha, mtafiti amebaini kuwa, licha ya riwaya ya *Rosa Mistika* kuwa na kurasa chache (kurasa 98) ina matumizi mengi ya maneno ya Biblia ukilinganisha na riwaya ya *Gamba la Nyoka*yenye kurasa 159. Hii inadhihirisha kuwa wingi wa kurasa si wingi wa matumizi ya maneno ya Biblia bali inategemea tukio lililokusudiwa kufikishwa kwenye jamii husika.

### 4.1.1 Matumizi ya Maneno ya Biblia katika Riwaya ya *Rosa Mistika*

Riwaya ya *Rosa Mistika* imetumia maneno kadha wa kadha ya Biblia katika kuhakikisha kwamba jamii inafikiwa na ujumbe na kwa namna ambayo itamfikirisha msomaji hasa katika kutafakari nini hasa lengo la mwandishi la kutumia maneno hayo. Riwaya hii imetumia maneno 16 lakini matini zilizoteuliwa ni 5. Hii ni kwa sababu sio maneno yote yaliyotumiwa yamebeba dhima fulani, hivyo, mtafiti ameteua maneno yale tu ambayo ameona yatawezesha kujibu maswali ya utafiti. Maneno ya Biblia yaliyobainika katika riwaya hii ni kama haya yafuatayo:-

#### 4.1.1.1 Kunyweni hii ndio damu yangu

Kunyweni hii ndio damu yangu ni maneno yanayopatikana katika kitabu Kitakatifu cha Biblia ambapo Yesu Kristo aliwaambia wanafunzi wake na kuwahimiza kufanya hivyo kama moja ya ukumbusho wake. Katika Imani ya Wakristo hususani Romani Katoliki Padri hubariki Ekaristi[1] kabla ya kuwapa waumini walioshiriki katika ibada ya misa Takatifu. Kwa kuzingatia imani ya Kikristo hususani Romani Katoliki, Ekaristi Takatifu ambayo ndio damu ya Yesu Kristo hainywewi na mtu yeyote yule bali hutumiwa na waumini ambao wameungama au wametubu dhambi zao na iwapo itatumiwa vinginevyo basi ni kinyume na taratibu na kanuni za imani za Wakristo na hivyo kuwa kama kejeli au dhihaka kwa Wakristo. Katika riwaya ya *Rosa Mistika* mwandishi ameonesha jambo hili pale anaposema:-

> Zakaria alikuwa amekwenda kusali kwenye pombe.
> Wanasema aliponunua pombe alizoea kuinua bakuli juu
> kuwapatia watu akisema, kunyweni hii ndiyo damu yangu (uk 16).

[1] Ekaristi ni sakramenti ya mwili na damu ya Yesu Kristo katika maumbo ya mkate na divai.

Kitendo cha Zakaria kunyanyua bakuli juu na kusema kunyweni hii ndio damu yangu kama ilivyojitokeza ukurasa wa 16 imetafsiriwa kama Yesu alivyochukuwa divai akanyanyua juu na kuwapa wanafunzi wake akiwaambia “kunyweni nyote, kwa maana hii ndio damu yangu ya agano”. Hivyo, Zakaria alitafsiri Biblia kwamba damu ndio pombe na watu waliokuwa wakinywa ile pombe kama wanafunzi wa Yesu Kristo. Yamkini Zakaria ni muumini wa dhehebu la Romani Katoliki, ndio maana alinyanyua juu lile bakuli kama ishara inayoonesha jinsi Padri anavyonyanyua juu kikombe cha divai wakati wa Ekaristi Takatifu.

Maneno haya aliyotumia mwandishi yanapatikana katika Biblia Takatifu kwenye kitabu cha Mathayo 26:27-28

> Akakitwaa kikombe, akashukuru, akawapa akisema, Nyweninyote katika hiki; kwa maana hii ndio damu yangu ya agano imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi

Maneno ya Mathayo 26:27-28 yanafanana na yale aliyoyasema mhusika Zakaria akiwa katika pombe. Kwa kurejelea nadharia ya uhemenitiki msingi wa imani inayodai kwamba matendo ya binadamu yanaathiriwa kwa njia mbalimbali na asasi tofauti zilizoko katika mazingira yake. Ukimwangalia mhusika Zakaria ameathiriwa na asasi ya dini katika dhehebu la Romani Katoliki kwani anaelewa vizuri matendo yanayofanywa na Padri wakati wa kubariki Ekaristi takatifu madhabahuni lakini kutokana na athari za pombe anaonekana kufanya matendo hayo nje ya madhabahu tena kilabuni kwa kebehi na hivyo

kusaidia wasomaji kuelewa kuwa katika jamii kuna watu wanaokebehi imani za watu wengine. Hivyo, mwandishi Euphrase Kezilahabi amemtumia Zakaria kuonesha jinsi watu wanavyoshindwa kujiheshimu baada ya kulewa hadi kufikia hatua ya kufanya matendo ya kukebehi yanayofanyika madhabahuni wakati wa ibada.

**4.1.1.2 Maskini wa Roho**

Maskini wa roho ni mtu ambaye anafanya matendo ambayo hayampendezi Mungu na hivyo kujikuta amefikia mahali ambapo hana imani tena na Mungu wake. Mwandishi ametumia maneno haya kuonesha mtu ambaye amekata tamaa, anamfadhaiko nafsini mwake, anakwenda katika njia isiyompendeza Mungu katika matendo yake. Mwandishi amemchora mhusika Rosa kama mtu anayefanya matendo yaliyokinyume na mapenzi ya Mungu kama vile uzinzi. Mwandishi amemtumia mhusika Padri kwenda kwa Rosa kwa lengo la kumsaidia kutubu dhambi zake na kumsaidia kurudisha tena tumaini lake kwa Mungu kwani Rosa bado ni wa thamani mbele za Mungu. Mwandishi amedhihirisha jambo hili pale anaposema;-

> Umekuja kunisaidia mimi maskini. Ndiyo, wewe maskini
> wa roho. Umejuaje, wewe Mungu? Mwovu huonekana kwa
> matendo (uk 48)

Kwa kurejelea mazungumzo ya Rosa na Padri, mwandishi ameonesha kuwa Rosa alimjua Mungu na alijua kuwa matendo yake ni chukizo mbele ya Mungu. Hivyo ujio wa Padri kwake ulikuwa ni moja ya njia ya kumwambia matendo yake hayampendezi Mungu na hivyo amwongoze sala ya toba ili arudi tena kumtumaini Mungu na kuacha matendo

mabaya. Katika imani ya Romani Katoliki, Padri amepewa uwezo wa kuondoa dhambi hivyo mwandishi alipomtumia Padri katika kumwondolea dhambi Rosa kilikuwa ni kile kinachofanywa na Mapadri katika dhehebu la Romani Katoliki. Maneno ya maskini wa roho yanapatikana katika Biblia katika kitabu cha Mathayo 5: 3 inasema "Heri walio maskini wa roho, Maana ufalme wa mbinguni ni wao". Maneno haya yanafariji na kuhamasisha waumini kutenda matendo mema, ili siku ya mwisho waweze kuurithi ufalme wa Mungu.Kwa kurejelea nadharia ya uhemenitiki msingi wa imani unaeleza kwamba matendo ya mwanadamu huathiriwa na asasi mbalimbali zilizoko katika mazingira yake. Tunamwona Rosa katika mazungumzo yake na Padri anafahamu ya kwamba Mungu yupo. Hili linadhihirisha kwamba asasi ya dini imemuathiri. Aidha kukubali ujio wa Padri ni njia mojawapo inayodhihirisha kwamba ni mfuasi wa dhehebu la Romani katoliki. Hivyo, ni dhahiri kwamba dhehebu la Romani Katoliki limemuathiri katika imani yake.

#### 4.1.1.3 KuungamaDhambi

Kuungama dhambi maana yake ni kuona uchungu na chuki moyoni juu ya dhambi utendazo na kukusudia kutokutenda tena. Kwa mujibu wa dhehebu la Romani Katoliki, Padri amepewa uwezo wa kuondoa na kusamehe dhambi. Kiimani na kiutaratibu wa dhehebu hili, kabla ya kwenda kuungama kwa Padri muumini anashauriwa kutatua matatizo yao nafsini mwao au na jirani yako kisha ndio aende kutubu kwa Padri kwa ajili ya ondoleo la dhambi. Hii imejitokeza pale Yesu Kristo aliposema katika maandiko yake kwenye Biblia Takatifu kuwa mwanadamu anapaswa kwanza kutatua tatizo lolote lile

kati yake na wanadamu wenzetu ili amani na utulivu viwepo na hivyo kuwa na uwezo wa kumwabudu Mungu katika dhamiri safi. Kwa mantiki hiyo, kuungama dhambi ni kumwambia Padri wazi wazi dhambi zako ulizotenda ili upate maondoleo ya dhambi na kusamehewa. Lengo la Padri kukuondolea dhambi ni kukurejeshea uhusiano wako mzuri na Mungu. Katika riwaya ya *Rosa Mistika* mwandishi anamchora mhusika Rosa pale ambapo alifikia uamuzi wa kunywa sumu ili kukatiza uhai wake baada ya kuona kwamba mchumba wake Charles hatamuoa tena ilhali yeye alimpenda sana kutokana na kumkuta hana bikira.Mwandishi anadhihirisha maneno haya pale anaposema "Rosa alifikiri kwanza kabla ya kunywa.Alitubu dhambi zake"(uk 91). Hivyo uamuzi wa Rosa kutubu dhambi zake ni kujiweka karibu na Mungu. Rosa alijua matendo yake yalikuwa ni chukizo mbele za Mungu na hata uamuzi wake wa kujiua ni chukizo kwa Mungu lakini mwandishi anaonyesha alitubu dhambi zake zote kabla ya kujiua.

Aidha, mwandishi anaendelea kuonesha jinsi Padri alivyokuwa na jukumu la kuwakumbusha Wakristo waliofika ibadani katika ibada ya mazishi ya Rosa, Zakaria na Regina ukuu wa Mungu ulivyomkubwa. Mwandishi anasema:-

> Alipofika penye maiti aliwanyunyizia
> maji ya Baraka na kusema, Kama
> ungezikumbuka dhambi,ee Bwana, nani,
> ee Bwana angesimama? (uk 94)

Kwa kurejelea maneno ya mwandishi ya ukurasa wa 94 hapo juu, inaonyesha na kudhihirisha kwamba Padri anawakumbusha waumini kutubu dhambi maana kwa Mungu kuna msamaha iwapo wanadamu watatubu dhambi zao. Mungu anawapenda wanadamu

na ndio maana hakumbuki dhambi zao hata kama zingekuwa kubwa namna gani, Mungu husamehe yote iwapo tu mwanadamu atakumbuka kutubu dhambi zake. Jambo la kukumbuka ni kwamba hakuna mtu aliyesafi mbele za Mwenyezi Mungu bali wote wanahitaji kutubu dhambi zao kwa kuwa hakuna dhambi kubwa na ndogo ama dhambi isiyosameheka mbele za Mwenyezi Mungu. Maneno hayo yanadhihirika katika Biblia kwenye kitabu cha Zaburi 130:3 pale inaposema “Bwana, kama wewe ungehesabu maovu, Ee Bwana, nani angesimama?” Maneno haya yanaonyesha huruma ya Mungu kwa wanadamu. Mungu ni mwingi wa rehema na humsamehe kila mtu amkimbiliaye kwa kufanya toba ya kweli.

Swala la kuungama dhambi limejitokeza pia katika riwaya ya *Gamba la Nyoka*, mwandishi anaonesha jinsi waumini walivyokwenda kwa Padri Madevu kuungama dhambi zao. Mwandishi anasema:-

> Kabla ya kuanza misa, padri Madevu alitupia
> macho upande wa wanawake; aliwaona wanawake
> fulani waliokuja kuungama dhambi zao juzi (uk 4).

Maneno haya yanadhihirika katika kitabu cha Biblia 1 Yohana 1: 8-9.

> Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe,
> wala kweli haimo mwetu.Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni
> mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha
> na udhalimu wote.

Nukuu hii ya Biblia inaonesha jinsi Wakristo wanavyopaswa kujutia makosa yao, kwani hutenda dhambi kwa kujua ama kutokujua. Hivyo, ni muhimu kwa Mkristo kufahamu

kuwa dhambi inatutenganisha na wokovu wa Mungu, hivyo inapaswa kuungama mbele za Mungu. Kwa kurejelea nadharia ya uhemenitiki, msingi wa imani ya kwamba matendo ya binadamu yanaathiriwa kwa njia mbalimbali na asasi tofauti zilizoko katika mazingira yake. Tukimwangalia mhusika Rosa katika riwaya ya *Rosa Mistika*na wale wanawake wawili katika riwaya ya*Gamba la Nyoka*waliokwenda kuungama kwa Padri Madevu, inadhihirisha kwamba wameathiriwa na imani ya dhehebu la Romani Katoliki. Hivyo, mwandishi Euphrase Kezilahabi amemtumia Rosa na wanawake wawili kuonesha jinsi asasi ya dini hususani imani inavyoweza kubadilisha matendo ya wanadamu.

**4.1.1.4 Kiti cha Enzi**

Kwa kurejelea imani ya Kikristo, kiti cha enzi ni nafasi ya juu ya utawala ambayo iko katika ulimwengu wa Kiroho wa Mungu chenye mamlaka juu ya mwelekeo wa maisha ya watu. Hii ni sehemu inayounganisha umoja wa kiroho wa Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu. Umoja huo ambao ndio unaotengeneza ufalme wa mbinguni unaunganishwa na kiti cha enzi ambacho ndicho chenye mamlaka yaani Mungu akiwa katika muunganiko wa nafsi zake zote tatu ambazo ni Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu. Mwandishi amemchora mhusika Rosa na Zakaria walipokuwa wanasomewa hukumu ya matendo yao duniani baada ya kukatisha uhai wao. Mwandishi anasema:-

> Mungu amekaa juu ya kiti chake cha Enzi.
> Malaika mmoja anapita amebeba karatasi
> ngumu iliyoandikwa juu yake kesi ya Rosa Mistika.
> Mungu: Rosa, kwa nini umejiua?
> Rosa: Ee Mungu wangu. Haya yote yametokea kwa sababu
> ya baba yangu. (Baada ya dakika moja, ZAKARIA anaingia.

Ana alama nyeusi kifuani. Anamsujudia MUNGU.
Mungu: Zakaria una usemi gani kujitetea?
Zakaria: Ee Mungu wangu. Haya yote yametokea kwa sababu ya ubaya na udhaifu wake mwenyewe!(uk 98)

Nukuu hii ya hukumu ya Rosa Mistika inayotolewa na Munguinaonesha kuwa udhaifu wa Rosa wa kiimani wa kutomjua Mungu namahangaiko ya duniani ndio yaliyosababisha ajiue na sio wazazi wake waliomsababishia yeye kujiua. Hali hii inadhihirisha kuwa kila mwanadamu baada ya kufa atahukumiwa. Mungu atakaa kwenye kiti chake cha enzi na kuhukumu kila mwanadamu kulingana na matendo yake aliyoyafanya duniani. Maneno haya yamejitokeza katika kitabu Kitakatifu cha Biblia kwenye Ufunuo wa Yohana 21:5 na Zaburi 103:1 ambayo yanasema:-

Na yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi akasema,
Tazama, nayafanya yote kuwa mapya.
Bwana ameweka kiti chake cha enzi mbinguni na
ufalme wake unavitawala vitu vyote.

Hii inamaana kuwa kiti cha enzi cha Mungu kipo na yeye hukitawala kwa vitu vyote ikiwemo kuhukumu mwanadamu baada ya kifo kama ambavyo mwandishi alivyoonesha juu ya hukumu ya mhusika Rosa Mistika na baba yake Zakaria baada ya kufa kwao.Kwa kurejelea nadharia ya uhemenitiki, msingi waimani ya kwamba matendo ya binadamu yanaathiriwa kwa njia mbalimbali na asasi tofauti zilizoko katika mazingira yake. Tunamwona mwandishi Euphrase Kezilahabi akiwachora wahusika Rosa na Zakaria wakisomewa hukumu yao. Hii inadhihirisha kwamba mwandishi anaamini kuwa kuna hukumu baada ya kifo. Matendo ya Rosa na Zakaria waliyofanya hapa duniani ikiwemo kujiua, yamesababisha kusomewa hukumu yao na Mwenyezi Mungu. Zakaria na Rosa

walifahamu kabisa ya kwamba Mwenyezi Mungu mtawala wa vitu vyote ndiye mtoa hukumu na ndio maana Zakaria alimsujudia Mungu alipokuwa akienda kusomewa hukumu yake.

#### 4.1.1.5 Utakatifu

Utakatifu ni usafi wa kiroho na kimwili;Tunapozungumzia usafi wa kiroho ina maana kwamba kuishi maisha ya wokovu, maisha yasiyokuwa na chuki, udhalimu, uchoyo, na mambo mengine yoyote yasiyomtukuza Mungu. Usafi wa kimwili ni kuwa nadhifu kimwili pamoja na mavazi. Mwandishi amemchora mhusikaRosa kama msichana mtulivu sana na mnyamavu alipokuwa akisoma katika shule ya wasichana ya Rosary. Rosa alikuwa mtu asiyependa kuongea mbele za watu, yeye aliongea kwa vitendo. Hali ya kutoongea ilimfanya aonekane Mtakatifu sana kwa watu lakini matendo yake yalimfanya aonekane malaya shuleni hadi kufikia hatua ya kuitwa "Lab yaani Laboratory". Kwa Kiswahili neno laboratory lina maana ya maabara yaani chumba au jengo lenye vifaa vya kufanyia majaribio ya kisayansi, utafiti wa kimatibabu, kufundishia, au kwa kuzalishia dawa au kemikali (BAKITA, 2016:74). Hivyo, Rosa alipewa jina hilo kutokana na tabia yake ya kujirahisisha mbele za wanaume. Mwandishi amethibitisha kauli hiyo kwa kusema:-

> Kumbe ndio maana uko mnyamavu namna hii!
> Ulifikiri tutafukuzwa? Utakatifu wako upo wapi? (uk 28)

Kauli hii ya ukurasa 28 ya mwandishi inaonyesha neno Utakatifu lilivyotumiwa na mwandishi kuwa, siku moja Rosa alitoroka na wenzake kwenda disko lakini kwa bahati mbaya walikamatwa na Sista na hivyo Rosa aliambiwa awataje wenzake aliotoroka nao.

Kitendo cha Rosa kuwataja wenzake kilimfanya achukiwe sana na wanafunzi wenzake aliotoroka nao kwenda disko na ndipo wanafunzi wenzie walipokasirika na kumwuliza Utakatifu wake uko wapi kama ameweza kuwataja wenzie ili wafukuzwe shule? Hii inaonyesha kwamba ukiwa mtakatifu au ukiwa na Utakatifu ndani yako unatarajiwa kuwa na roho ya huruma kwa wenzako na usafi wa moyo, na mara unapokubwa na tatizo la kufanya makosa unakubali kubeba mzigo wa wenzako kwa lengo la kuwasaidia. Hivyo Rosa alitakiwa kutowataja wenzake na badala yake kuubeba mzigo huo mwenyewe kwa ajili ya wenzake ikiwemo kuomba msamaha kwa sista kwa kosa alilolitenda na kukubali adhabu yoyote atakayopewa kwa ajili ya kuwaokoa wenzake. Nukuu ya utakatifu imejitokeza pia katika Biblia Takatifu kwenye kitabu cha waraka wa kwanza wa Petro1:15-16

> Bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu,
> ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote.
> Kwa maana imeandikwa, mtakuwa watakatifu kwa kuwa
> mimi ni mtakatifu.

Nukuu hii ya maneno ya kwenye Biblia inadhihirisha kuwa inabidi tujitakase yaani kufanya toba pale tunapofanya makosa au matendo mabaya ya kumchukiza Mungu ili tuweze kuwa watakatifu kama yeye Mungu alivyo mtakatifu. Kwa kurejelea nadharia ya uhemenitiki, msingi wa utukuzaji unasema kuwa msomaji huwa na makisio mbalimbali pindi tu aisomapo kazi ya fasihi kutokana na jina la kitabu, kiwango cha usomi au upeo wa uelewa. Yaelekea Rosa alichukuliwa na wanafunzi wenzake mtakatifu, hivyo asingeweza kusababisha wenzake kupewa adhabu ama kufukuzwa shule kutokana na kosa walilofanya. Mtazamo waliokuwa nao wanafunzi wenzake kumbe ilikuwa ni

kinyume chake hali iliyosababisha wamchukie Rosa kwa kuhusianisha matendo ambayo mtu ambaye ni mtakatifu anayotakiwa kutenda.

### 4.1.2 Matumizi ya Maneno ya Biblia katika Riwaya ya *Gamba la Nyoka*

Riwaya ya *Gamba la Nyoka* imebainika kutumia maneno ya Biblia katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Riwaya hii imetumia maneno ya Biblia 12 lakini maneno yaliyoteuliwa ni 4 kutokana na kukidhi malengo ya utafiti. Pamoja na riwaya hii kuwa na kurasa 159, ni kurasa 13 tu ambazo zimebainika kutumia maneno ya Biblia. Maneno ya Biblia yaliyotumika ni kama ifuatavyo:-

#### 4.1.2.1 Damu yao na iwe juu ya Vichwa vyenu, mimi nanawa mikono kama Pilato

Ndani ya Biblia Takatifu maneno haya yalitumiwa na Pilato wakati alipowauliza wakuu wa Makuhani kati ya Yesu na Baraba yupi wanayetaka afunguliwe? Ndipo wakuu wa Makuhani walipojibu Baraba afunguliwe na Yesu asulubiwe. Pilato alinawa mikono akimaanisha kupingana au kutokushiriki au kutokuhusishwa na jambo linalotendeka, na endapo litakuwa na hatia yoyote basi yeye hatatiwa hatiani kwani hakushiriki kufanya au kutenda jambo hilo. Katika riwaya ya *Gamba la Nyoka*mwandishi anatumia maneno haya pia pale anaposema:-

> Napinga kabisa unyama huu!Nashukuru kuwa mimi sitakuwapo.
> Damu yao na iwe juu ya vichwa vyenu. Mimi nanawa
> mikono kama Pilato (uk 28)!

Kwa kurejelea maneno ya mwandishi katika ukurasa wa 28 hapo juu, Mamboleo anaonekana kupingana na shambulio lililopangwa kufanyika kati ya wanakijiji wa Kisole na wanamgambo, ambapo wanamgambo pamoja na maaskari wengine waliuawa hali iliyosababisha kujipanga kwa ajili ya shambulio lingine. Katika mipango hiyo, Mamboleo anaonekana kutokuwa tayari kwa ajili ya umwagaji damu kwa watu aliowaona hawana hatia yoyote. Hapo ndipo Mamboleo alisema "ananawa mikono kama Pilato" akimaanisha kwamba hatahusika na lolote litakalotokea katika Kijiji cha Kisole.Katika Biblia Injiliya Mathayo Mtakatifu 27:22-25 inasema:-

> Basi Pilato alipoona ya kuwa hafai lolote, bali ghasia inazidi tu. Akatwaa maji, akanawa mikono yake mbele ya mkutano, akasema, mimi sina hatia katika damu ya mtu huyumwenye haki; yaangalieni haya ninyi wenyewe. Watu wote wakajibu wakasemadamu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu.

Dondoo hiyo hapo juu inaonesha jinsi Pilato alivyonawa mikono na laana yoyote juu ya kumuua Yesu. Kwa kurejelea nadharia ya uhemenitiki msingi wa imani inayodai kwamba matendo ya binadamu yanaathiriwa kwa njia mbalimbali na asasi tofauti zilizoko katika mazingira yake. Ukimwangalia mhusika Mamboleo anaonekana kwamba anafahamu fika kwamba kuuwa ni dhambi na hata imani katika maandiko matakatifu imekataza. Kutokana na imani yake ndio maana hakutaka kujihusisha na shambulio la kuuwa wanakijiji lililopangwa kufanyika kijijini kwake. Hivyo, matendo yake yalidhihirisha kwamba dini imemuathiri kwani aliweza kujinasibisha kama ambavyo Pilato alivyonawa mikono wakati wa kumuua Yesu.

#### 4.1.2.2 Baba Ikiwezekana Kikombe hiki Kinipite

Baba ikiwezekana kikombe hiki kinipite ni maneno yaliyosemwa na Yesu Kristo wakati akielekea kwenye mateso bustani ya Gethsemane na pia yamejitokeza katika riwaya ya *Gamba la Nyoka.* Katika riwaya ya *Gamba la Nyoka* maneno haya aliyasema mama Tinda alipokuwa akimwomba Mungu amkingie na bomoabomoa iliyokuwa ikipita kupisha vijiji vya ujamaa, akijua hata atakapopata sehemu nyingine watakayogawiwa hana uwezo wa kujenga. Haya yanadhibitishwa pale mwandishi anaposema:-

> Wachape hao watakaozibomoa. Wewe ulilia: Baba, ikiwezekana kikombe hiki kinipite!nami nalia:' Mungu ikiwezekana kikombe hiki cha vijiji vya ujamaa kinipite! (uk 3)

Aidha, katika Biblia Takatifu maneno ya mama Tinda yanajitokeza katika Injili yaMathayo Mtakatifu 26: 39 inasema

> Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifulifuli, akaomba akisema, Baba yangu, ikiwezekana kikombe hiki kiniepuke walakini si kama nitakavyo mimi, bali mapenzi yako yatimizwe.

Halikadhalika injili ya Luka Mtakatifu 22:41-42 inasema

> Mwenyewe akajitenga nao kama kiasi cha kutupa jiwe,akapiga magoti akaomba akisema, Ee Baba ikiwa ni mapenzi yako, uniondolee kikombe hiki; walakini si mapenzi yangu bali yako yatendeke.

Nukuu hii ya Mathayo na Luka inaendana na maneno ambayo mama Tinda aliyasema akihitaji msaada wa Mungu ili kuzuia nyumba yake kubomolewa.Kwa kurejelea msingi wa nadharia ya Uhemenitiki ambao ni imani ya kwamba mwanadamu anaathiriwa na asasi mbalimbali zilizoko katika mazingira yake. Tunamwona mama Tinda akiomba msaada wa Mungu, hii inadhihirisha kwamba anamwamini Mungu kwamba anaweza

kumwokoa katika jambo lolote na hivyo anafananisha kuepuka kwa tukio la kubomolewa nyumba na kikombe ambacho Yesu Kristo aliomba kisimpate. Jambo hili linadhihirisha kwamba mama Tinda ameathiriwa na dini kwani anaamini ya kwamba Mungu anaweza kumuepusha na balaa la kubomolewa nyumba.

#### 4.1.2.3 Kwa Jina la Baba, na Mwana na la Roho Mtakatifu

Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu ni maneno ambayo Padri huyatumia kabla ya kuanza Ibada, wakati wa ubatizo, wakati wa sakramenti ya upatanisho, wakati wa sakramenti ya ndoa na kabla ya sala yoyote ambapo huanza kwa jina la Utatu Mtakatifu, yaani Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu. Utatu Mtakatifu yaani Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu ni nafsi tatu za Mungu mmoja zote ni sawa katika uasili. Utatu mtakatifu ni fumbo la imani kuwa katika Mungu mmoja kuna nafsi tatu yaani Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu (Ighondo, 2019). Mwandishi anadhibitisha haya pale anaposema:-

> Alipoanza kuvuta hamu ya kusali. Alitazama juu kwa Mungu na kisha akaanza kwa jina la Baba...(uk 4)Wakristo wapenzi, kutaneni mjadili suala hili la kuhama,Mkiwa na sauti moja Mungu anaweza kuwasaidia... Kwa jina la Baba, la Mwana na la Roho Mtakatifu, Amina.(uk 6)

Kwa kurejelea nukuu ya ukurasa wa 6, Padri Madevu alianza ibada kwa kuita Utatu Mtakatifu kama ilivyo kanuni na taratibu za dhehebu la Romani Katoliki. Ukihusianisha na utaratibu huo maneno haya ya Utatu Mtakatifu yamejitokeza katika Biblia Takatifu kwenye Injiliya Mathayo Mtakatifu 28:19

> Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi,

mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu.

Nukuu hiyoinaonesha Yesu akiwatuma wanafunzi wake kuwabatiza watu wote ili kufanya mataifa yote kuwa watoto wake kwa kuwabatiza kwa jina la Utatu Mtakatifu. Kwa kurejelea nadharia ya Uhemenitiki, msingi wa utukuzaji unadai kuwa ni jumla ya makisio mbalimbali ambayo msomaji au mhakiki wa kazi ya fasihi huwa nayo punde aishikapo kazi yoyote ya fasihi, yakiongozwa na utamaduni, kiwango cha usomi, upeo wa uelewa. Kitendo cha Padri Madevu na mama Tinda kupiga ishara ya Utatu Mtakatifu kinadhihirisha kwamba huo ni utamaduni wa dhehebu la Romani Katoliki unaotumiwa duniani kote. Hii inadhihirisha kwamba dhehebu la Romani Katoliki asili yake ni Roma, hivyo taratibu zote zinazotumiwa na Padri ikiwemo ishara ya Utatu Mtakatifu ni utaratibu unaotoka Roma chini ya uongozi wa Papa. Hivyo, mama Tinda na Padri Madevu wanafuata utamaduni uliozoeleka kutumiwa na dhehebu hili duniani kote.

#### 4.1.2.4 Maria,mama wa Mungu aliyezaa kwa nguvu za Roho Mtakatifu

Maria, mama wa Mungu aliyezaa kwa nguvu za Roho Mtakatifuni maneno yanayopatikana katika Biblia Takatifu na pia yametumiwa katika riwaya ya *Gamba la Nyoka.*Katika riwaya ya *Gamba la Nyoka*maneno hayo yamejitokeza pale mama Tinda alipoenda mbele ya Mwenyezi Mungu ili kuweza kuzungumza nae ya moyoni mwake.Mama Tinda alimwomba Mungu amsaidie kupitia malaika wake na Maria mama wa Mungu asipatwe na balaa la bomoabomoa. Maombi ya kupitia malaika wa Mungu na Bikira Maria mama wa Mungu ni moja ya utamaduni wadhehebu la Romani Katoliki.

Kulingana na imani ya dhehebu hilo, mama Maria anapewa heshima kubwa hata kuweza kupewa uwezo wa kuwaombea watu kwa mwanae Yesu Kristo.Vivyohivyo, mama Tinda aliomba kwa Mungu kupitia mama wa Mungu Bikira Maria, aweze kumwombea kwa mwanaye Yesu Kristo amuepushe na balaa la kuvunjiwa nyumba kwa ajili ya kuanzishwa kwa vijiji vya ujamaa. Hayo yanadhihirishwa na mwandishi pale anaposema:-

> Moyo wake ulianza kudunda, alikuwa na jambo la maana sana
> moyoni, jambo la kumwambia Mungu na Malaika wake.
> Hakumsahau Maria, mama wa Mungu aliyezaakwa nguvu
> za Roho Mtakatifu...(uk 1)

Heshima ya Bikira Maria mama wa Mungu imejitokeza pia katika Biblia Takatifu kwenye Injili ya Luka Mtakatifu 1:26-44 inasema

> Mwezi wa Sita, malaika Gabrieli alitumwa na Mungu kwenda mpaka
> mji wa Galilaya, jina lake Nazareti, kwa mwanamwali bikira
> aliyekuwa ameposwa na mtu, jina lake Yosefu jina la bikira
> huyoni Mariamu.Tazama, utachukua mimba na kuzaa
> mtoto mwanamume, na jina lake utamwita Yesu...
> Mariamu akamwambia malaika, litakuwaje neno hili
> maana simjui mume?Malaika akajibu akamwambia roho
> Mtakatifu atakujilia juu yako...

Nukuu hiyo hapo juu kutoka katika kitabu cha Luka Mtakatifu 1:26-44 inaonesha jinsi malaikaalimwendea Maria na kumpa habari njema kwamba atapata mimba na kitakachozaliwa kitakuwa Kitakatifu. Maria alimzaa mkombozi wa dunia Yesu Kristo. Pamoja na kwamba Maria alikuwa na mumewe Yosefu bado alibaki kuwa Bikira kwani hakupata kumjua mwanamume yeyote.Kwa kurejelea msingi wa imani katika nadharia ya uhemenitiki unadai kuwa matendo ya mwanadamu yanaathiriwa na asasi mbalimbali zilizomo katika mazingira yake. Kitendo cha mama Tinda kumuomba Mungu kupitia mama wa Mungu Maria, ni imani iliyojengeka ndani yake, ya kwamba yampasa

kumwomba mama wa Mungu bikira Maria ili aweze kumwombea kwa mwanae Yesu Kristo. Hivyo, mama Tinda ameathiriwa na dini ya dhehebu la Romani Katoliki linaloamini kwamba ili maombi yako yasikilizwe yapasa kumwomba mama wa Mungu akuombee kwa mwanaye Yesu Kristo.

## 4.2 Dhima za Matumizi ya Maneno ya Biblia katika Riwaya ya *Rosa Mistika* na*Gamba la Nyoka*.

Hili lilikuwa lengo la pili la utafiti ambalo lililenga kueleza dhima za matumizi ya maneno ya Biblia yaliyobainika katika lengo la kwanza. Katika kuhakikisha kwamba lengo hili linafikiwa, mtafiti alisoma riwaya teule kwa umakini na kwa kufanya marudio katika kuhakikisha kwamba anapata kile ambacho kimebebwa na maneno ya Biblia aliyotumia mwandishi kuifikishia jamii ujumbe. Hivyo, katika kuchunguza maneno ya Biblia yaliyotumika, mtafiti amebaini dhima mbalimbali kama zilivyojadiliwa hapa chini:-

### 4.2.1 Kulea Watu Kiroho

Mwandishi ametumia maneno ya Biblia yanayodhihirisha namna maneno ya Biblia yanavyoweza kutumiwa na viongozi wa dini katika kuwakuza na kuwalea waumini kiroho. Mwandishi Euphrase Kezilahabi katika *Rosa Mistika*amemtumia Padri kubeba jukumu la kulea watu kirohokama mistari ifuatayo inavyosema;-

> "Mimi mtumishi wa Mungu. Nimekuletea habari njema, Rosa.

> Padri alifungua Biblia yake, pale alipokuwa ameweka picha ya mtu msalabani. Rosa alijaribu kusikiliza Padri alipoanza kusoma. John 8. 1-10, Walikwenda kila mtu nyumbani kwake,naye Yesu akaenda mpaka mlima wa mizeituni. Hata asubuhi kulipokucha akaingia tena hekaluni, na watu wote wakamwendea; naye akaketi, akawa akiwafundisha. Waandishi na Mafarisayo wakamletea mwanamke aliyefumaniwa katika uzinzi, wakamweka katikati. Wakamwambia...” Padri alisoma mpaka mwisho. Alisoma maneno ya mwisho tena. Yesu akawaambia, wala mimi sihukumu. Enda zako walausitende dhambi tena.” ( uk 49)

Dondoo hili linaonesha jinsi maneno ya Biblia yanavyoweza kutumiwa kumfariji mtu na kumpatia miongozo ya kweli katika maisha. Zana muhimu ambayo kiongozi wa dini anapaswa kuwa nayo ni Biblia. Kupitia Biblia hiyo ndipo inapopatikana mistari ya kiroho ambayo kwa namna ya pekee ikitumiwa vizuri katika mafundisho yake na walezi wa kiroho huweza kujenga jamii yenye maadili mema. Hivyo ndivyo Rosa alipaswa kusaidiwa kupitia Padri ili aweze kubadilika na kurudi katika kutenda matendo mema yanayopendeza jamii na Mungu kwa ujumla.

Vilevile katikakitabu cha *Gamba la Nyoka* mwandishi amemtumia Padri Madevu kuonesha jinsi viongozi wa dini walivyokabidhiwa jukumu kubwa la kulea watu kiroho. Mwandishi anasema:-

> “...aliwaona wanawake fulani waliokuja kuungama dhambi zao juzi...Nilitembea na Padri Johnson mara nne, Padri Johnson alikuwa Padri mwenzake katika parokia hiyo. Nilicheka kilema mara kumi... aligeuza kichwa haraka na kutazama upande wa wanaume, Upande huo alimwona kijana mmoja aliyeungama kuwa anatembea na mke wa katekista (uk 4)
>
> Injili ya Mt Luka yaendelea 21: 25-33 Siku ile Yesu aliwaambia wafuasi wake zitakuwako ishara katika jua na mwezi, na nyota, na katika nchi mashakaya mataifa kwa ajili ya mshindo wa

> bahari na mawimbi...mwanawa Mungu akija katika wingu,
> mwenye nguvu na utukufu mwingi.(uk 5)

Dondoo hili hapo juu linaonesha jinsi Padri anavyotumia hekima katika kufikisha neno la Mungu kwa waumini kwa kutumia maneno ya Biblia. Malezi ya kiroho yanaendana na imani aliyonayo mtu. Pasipokuwa na imani ni vigumu kutoa mafundisho yatakayobadilisha mienendo ya watu katika jamii. Kutokana na imani waliokuwa nayo watu ndio maana walienda kuungama dhambi zao kwa Padri, na kupitia imani hiyo ndio pale wanapoamini kuwa baada ya kuungama dhambi unasamehewa na Mungu.Kwa kurejelea nadharia ya uhemenitiki msingi wa imani inayodai kwamba matendo ya binadamu yanaathiriwa kwa njia mbalimbali na asasi tofauti zilizoko katika mazingira yake. Kitendo cha wanawake wawili kuungama dhambi kwa Padri ni matokeo ya imani ya kwamba wameathiriwa na dhehebu la Romani Katoliki. Vilevile kitendo cha Rosa kukubali ujio wa Padri nyumbani kwake kinadhihirisha imani yake kuwa Mungu yupo.

### 4.2.2 Kukejeli

Kejeli ni tendo au kauli ya kukebehi, kubeza au utani azitoazo kwa mtu mwingine (BAKITA, 2016:408) Tukirejelea baadhi ya maneno yaliyotumika kama yalivyobainishwa katika lengo la kwanza, tunaona kwamba kejeli imejitokeza katika riwaya zote. Kwa kuanza na riwaya ya *Gamba la nyoka* mwandishi anaonesha jinsi mama Tinda alivyokuwa akisali kwa Mungu kupitia mama Bikira Maria ambaye ni mama wa Mungu alivyokuwa akitumia maneno ya kukebehi katika maombi yake. Mwandishi anasema;

> "Aliutazama kwa wasiwasi ule mraba wenye pembetatu na macho matatu. Hakuwa na uhakika kama huyoalikuwa Mungu kweli au zimwi. Alikumbuka hadithi alizosimuliwa zamani na bibi yake. Alianza kusali,macho matatu! Wewe unaona kila mahali. Wamulike hao wenye mioyo ya wivu. Wameze...Hakuweza kuendelea;hakuwa na uhakika alikuwa akisali kwa nani. Alihama na kuiendea ile picha ya Bikira Maria. Alipiga magoti, akaanza kusali; Maria Bikira, uliyekuwa Bikira hata baada ya kuzaa, ninakuomba unisikie. Isikie sauti ya mke mwenzako".(uk 3)

Dondoo hili linaonesha jinsi mama Tinda alivyotumia maneno ya kebehi katika kusali kwani kitendo cha kumwita Bikira Maria kwamba 'mke mwenzake' haipendezi na kitendo hicho kinaonekana kwamba ni kebehi. Mama Bikira Maria amepewa heshima kubwa kulingana na dhehebu la Romani Katoliki, hivyo, mama Tinda hakupaswa kujifananisha na mama Bikira Maria kwa namna yeyote ile.

Halikadhalika, katika riwaya ya *Rosa Mistika* kejeli imeonekana pale ambapo Zakaria alipozoea kwenda kunywa pombe kilabuni na baada ya kulewa ananyanyua bakuli juu kama Padri anavyobariki Ekaristi Takatifu wakati wa ibada kabla ya kugawa kwa Wakristo waliojiandaa kushiriki Ekaristi Takatifu. Kitendo cha Zakaria kuinua juu bakuli na kusema "kunyweni hii ndio damu yangu"ni kejeli kubwa sana kwa Wakristo wa dhehebu la Romani Katoliki na kanisa kwa ujumla kwani aliifananisha pombe na Ekaristi Takatifu ambayo ni Damu ya Yesu Kristo. Kiimani aliyepewa mamlaka ya kubariki Ekaristi ni Padri pekee, na si mtu mwingine yeyote. Ukirejelea nadharia ya uhemenitiki msingi wa imani unadai kwamba matendo ya binadamu yanathiriwa na asasi tofauti zilizopo katika mazingira yake. Tunamwona mama Tinda alivyoathiriwa na dini kwani

anaonesha kwamba anaamini ya kuwa Yesu Kristo amezaliwa na Bikira Maria lakini kitendo chake alichoonesha ni kejeli. Aidha, hili linadhihirika pia kwa mhusika Zakaria kwani anaigiza kitendo cha kunyanyua bakuli juu kama Padri anavyobariki Ekaristi akiwa madhabahuni huku akijua kuwa ni kinyume na maandiko. Hivyo, inaonesha kwamba Zakaria na mama Tinda wameathirika na imani ya dini ya Romani Katoliki kiasi cha kuanza kufanya matendo ambayo yako kinyume na dhebehu hilo.

### 4.2.3 Kufariji Watu Waliokata Tamaa

Kukata tamaa ni hali ya kushindwa au kuona kwamba jambo fulani haliwezekani kufanywa ingawamhusika Padri kufariji watu wanaoonesha kukata tamaa kutokana na hali ngumu ya kimaisha wanayopitia. Mfano mzuri mwandishi anatuonesha jinsi mama Tinda alivyokuwa anakatishwa tamaa na mambo yaliyokuwa yakiendelea kijijini kwake. Mwandishi anadhihirisha suala hili pale anaposema:-

> "Siku ile: Yesu akawambia wafuasi wake: zitakuwako ishara
> katika jua, na mwezi, na nyota; na katika nchi mashaka ya mataifa
> kwa ajili ya mshindo wa bahari na mawimbi. Watu wakivunjika
> moyo kwa hofu, na kwa kuyatazamia mambo yatakayoupata
> ulimwengu; kwa maana nguvu za mbingu zitatikisika. Ndipo
> watakapomwonaMwana wa Adam akija katika wingu,
> mwenye nguvu na utukufu mwingi..." (uk 5)

Ukirejelea nukuu ya ukurasa wa 5 inaonesha jinsi maneno ya Biblia yanavyotumika katika kufariji watu waliokata tamaa na kuwafanya wasivunjike moyo wala kukata tamaa hali ambayo inamfanya mtu kushindwa kutimiza malengo yake.

Halikadhalika, katika riwaya ya *Rosa Mistika,* mwandishi amemtumia mhusika Padri kurudisha matumaini kwa Rosa baada ya kuonekana kwamba amekata tamaa kutokana na maisha aliyoishi. Rosa alikuwa amechoshwa na dunia, anaiona dunia imemwingiza katika matatizo makubwa ambayo hawezi kusaidika kwa namna yeyote. Pamoja na Padri kumfuata Rosa ili amhubirie habari njema za wokovu, Bado Rosa anaonekana kukata tamaa. Padri aliendelea kumsomea mistari ya Biblia ili kumdhihirishia kwamba bado lipo tumaini, bado ana nafasi ya kutubu mbele za Mungu na kurejesha tena furaha yake. Mwandishi anasema:-

> "Walikwenda kila mtu nyumbani kwake, naye Yesu
> akaenda mpaka mlima wa mizeituni. Hata asubuhi kulipokucha
> akaingia tena hekaluni, na watu wote wakamwendea; naye akaketi,
> akawa akiwafundisha. Waandishi na Mafarisayo wakamletea
> mwanamke aliyefumaniwa katika uzinzi, wakamweka
> katikati. Wakamwambia..." Padri alisoma mpaka mwisho.
> Alisoma maneno ya mwisho tena. Yesu akawaambia,
> wala mimi sihukumu. Enda zako wala usitende dhambi tena".(uk 49)

Nukuu hiyo inayopatikana ukurasa wa 49 inaonesha jinsi maneno ya Biblia yanavyotumika kufarijiwatu waliokata tamaa, kutia moyo, kuleta hamasa, na kurejesha tumaini kwa watu waliokata tamaa kutokana na changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo katika maisha. Padri alimtolea mfano mwanamke mwasherati alivyoweza kusamehewa pamoja na kuona kwamba ametenda kosa kubwa zaidi mbele za Mungu, hivyo ndivyo alivyomsihi Rosa asikate tamaa kwani hakuna dhambi kubwa mbele za mwenyezi Mungu.Ukirejelea nadharia ya uhemenitiki msingi wa utukuzaji unaeleza kwamba msomaji huwa na makisio pindi aishikapo kazi ya fasihi akihusisha na upeo wa

uelewa, utamaduni na kiwango cha usomi. Msingi huu unamtaka msomaji kutumia upeo wa uelewa katika kutafakari matini. Tunaona maandiko ya Biblia yanavyohimiza na kuwatia moyo watu waliokata tamaa, halikadhalika Padri ndivyo alivyochukua kifungu katika mistari ya Biblia katika kutimiza azma yake ya kuwatia moyo waumini wake. Hii inadhihirisha kwamba yanayotendwa na viongozi wa dini ndio yaliyoandikwa katika vitabu vitakatifu kama vile Biblia na Kuruani.

### 4.2.4 Kuonesha Unafiki wa Viongozi wa Dini

Viongozi wa dini wamewekwa kwa ajili ya kuongoza watu na kuwakuza katika misingi ya imani zao. Inapotokea kiongozi huyo kufanya matendo ambayo ni kinyume na mafundisho wanayofundisha huonekana kuwa wanafiki. Kwa mujibu wa BAKITA (2016:1131) Unafiki ni dai la uongo au la kujifanya kuwa unafuata taratibu, misingi ya uadilifu, urafiki au imani ilihali ni kinyume chake. Mwandishi Euphrase Kezilahabi katika kitabu cha *Rosa Mistika* anamtumia mhusika Padri kwenda nyumbani kwa Rosa kwa ajili ya kumfariji na kumrudisha tena katika maisha ya wokovu na yale yanayoipendeza jamii. Padri anaonekana kushindwa kutimiza wajibu wake kama kiongozi wa dini kwani kitendo chake cha kutoka nje kwa kasi na Biblia yake kwapani kunadhihirisha kwamba yeye mwenyewe amekata tamaa ndiyo maana aliondoka kwa Rosa.Mwandishi anasema;

> Padri, maishayangu yamekwishaharibika,na sijali! Kwa nini wewe ujali rohoyangu kuliko mimi mwenyewe? Padri alimwangalia, alishangaa. Alisimama na kufungua mlango. Kabla ya kutoka nje alisema: “Lusifa! Lusifa! Amekwishafanya roho yako kiti chake”. Padri alionekana akitoka nje kasi sana na Biblia yake kwapani. Rosa alifunga mlango. Hakuzidi tena

> kumwona Padrihuyo kwa siku zilizofuata (uk 49).

Nukuu hiyo hapo inaonesha jinsi viongozi wa dini wanavyokuwa walaghali kwa maana kwamba wanashindwa kutimiza majukumu yao. Kitendo cha Padri kumwambia Rosa "Lusifa! Lusifa! Amekwishafanya roho yako kiti chake" inadhihirisha kwamba ni unafiki wa viongozi wa dini kwani hakutakiwa kusema maneno hayo mbele ya Rosa bali alitakiwa kuendelea kuomba kwa ajili yake tena kwa toba kuu.

Halikadhalika, katika kitabu cha *Gamba la Nyoka* mwandishi anaonesha jinsi viongozi wa dini walivyowanafiki kwa kufundisha yale ambayo hata wao wenyewe kuyatenda yanakuwa vigumu kwao. Padri Madevu anaonekana kuvunja amri ya sita na amri ya kumi kama mwandishi anavyotuonyesha:-

> "Leo nimekuletea tena vidonge vingine. Vile vingine nafikiri vimekaribia kwisha". Padri Madevu alisema hali akifungua mkoba wake kutoa hivyo vidonge. "Ukiendelea kumeza vidonge hivi hatutapata aibu ya aina yoyote ...Lazima tujitahidi kutunza heshima ya majina yetu," Padri Madevu alisema hali akimsogelea. "Hebu nifunge mlango , Mama Tinda alisema akiinuka.(uk 7)

Ukirejelea mazungumzo kati ya Padri Madevu na mama Tinda hapo juu inaonesha jinsi Padri Madevu alivyokuwa akizini na mama Tinda. Akimpelekea vidonge vya kuzuia mimba ili asije akapata mimba ikawa aibu katika kanisa kwani Padri anatakiwa kuishi kwa kufuata mfano wa Yesu Kristo kwa kutokuoa wala kuwa na watoto. Kwa misingi hiyo Padri alivunja amri za Mungu ambazo alitakiwa kuzisimamia na kuwafundisha watu kuzishika na kuishi kulingana na amri hizo. Hivyo ndivyo viongozi wa dini

wanavyoonekana wanafiki kwa kushindwa kuishi maisha wanayofundisha. Mwandishi anaendelea kuonesha unafiki wa viongozi wa dini pale anaposema;

> "Napika. Mama Tinda alisema sasa kwa macho ya kurembuka. Picha ya Bikira Maria, saa ya mkononi na chupa ya marashi- Mungu ampe nini?...Saa kumi na mbili, Padri madevu alikuwa sasa ameketi tena kwenye kiti sebuleni..."Mungu akubariki kwa wema na ukarimu wako unaowafanyia watumishi wake." Kisha kwa mkono wake wa kulia alikatakata hewa. Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu" alimaliza kwa sauti nzito ya kinabii.(uk 9)

Mwandishi amemchora Padri Madevu alivyokuwa na uhusiano wa kimapenzi na mama Tinda ambapo alikuwa akimpelekea zawadi mbalimbali ili kuimarisha uhusiano wao. Padri Madevu anafundisha watu kuachana na uzinzi na haswa kuzishika amri za Mungu wakati yeye anashindwa kuishi katika mafundisho anayoyatoa. Kwa mantiki hiyo huo ni unafiki.Ukirejelea nadharia ya uhemenitiki msingi wa utukuzaji unaeleza kwamba msomaji huwa na makisio mbalimbali pindi aishikapo kazi ya fasihi. Makisio hayo hujengwa na kiwango cha usomi, utamaduni na upeo wa uelewa. Tunamwona Padri Madevu akishindwa kutimiza wajibu wake pamoja na kwamba alikuwa na nafasi kubwa katika kubadilisha maisha ya watu. Padri Madevu ni mfano wa viongozi wanaopewa mamlaka ya kuongoza watu kiroho na kushindwa kutimiza wajibu wao.

### 4.3 Athari za Maneno ya Biblia Yaliyotumika katika Riwaya ya R*osa Mistika* na *Gamba la Nyoka* kwa Wakristo

Lengo la tatu na la mwisho katika utafiti huu ni kubainisha athari za matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka* kama tulivyobainisha

malengo mahususi katika sura ya kwanza. Ili kutimiza lengo hili mtafiti alisoma kwa umakini riwaya teule ili kuweza kubaini endapo maneno ya Biblia yaliyobainika katika riwaya hizo yanaathari yoyote kwa Wakristo kutokana na jinsi mwandishi Euphrase Kezilahabi alivyoyatumia katika vitabu vyake. Hivyo, mtafiti alibaini kwamba, maneno ya Biblia yanapotumiwa yanaweza kuwa na athari hasi au chanya kwa Wakristo kulingana na namna maneno hayo yanavyotumika. Zipo athari ambazo zimeweza kujitokeza kutokana na matumizi ya maneno ya Biblia kwa Wakristo. Athari hizo ni kama hizi zilizojadiliwa hapa chini.

### 4.3.1 Kutokuwa na Imani na Viongozi wa Dini

Moja ya athari ambazo zinaweza kutokana na matumizi ya maneno ya Biblia kwa Wakristo ni pamoja na Wakristo kukosa imani na viongozi wao wa dini. Kwa kumtumia mhusika Padri katika kitabu cha *Rosa Mistika*, mwandishi Euphrase Kezilahabi amemchora mhusika Padri kuwa kashindwa kutimiza wajibu wake kama kiongozi mwenye dhamana ya kulinda na kuokoa watu katika mambo magumu wanayokutana nayo. Pamoja na wajibu mkubwa alionao Padri bado anaonekana kushindwa kulinda nafasi yake kwa watu anaowaongoza. Wakristo wanaonekana kumwamini Padri kama kiongozi anayeweza kutetea, kuwasaidia na kuwalisha kiroho. Padri anaonekana kushindwa kutimiza wajibu wake na hivyo kuwafanya Wakristo kuwa na wasiwasi nae na kushindwa kuwa na imani thabiti juu ya yale mafundisho anayoyatoa. Mwandishi anaonesha suala hili pale ambapo Padri alienda kumsaidia Rosa kuachana na maovu ya dunia na kuweza kumrudia Mungu lakini anaonekana kushindwa kumrejesha tena Rosa

katika maisha mapya ya kumtegemea Mungu. Swali la kujiuliza ni; Je! Kama Padri mtumishi wa Mungu ameshindwa kumbadilisha Rosa kuachana na mambo ya dunia, nani mwingine atakayeweza kumbadilisha? Mwandishi anasema,

> Rosa nimekuja kukusaidia;nimekuja kukuonesha tena mwanga wa wokovu umekuja kunisaidia! kwani mimi maskini? umejuaje, wewe Mungu?...Rosa alianza kutapika maneno,na matapishi hayamezwi tena.Wokovu maana yake nini?Wokovu! Wokovu gani!
> Kama kuna moto basi nitakwenda...Padri alimwangalia, alishangaa. Alisimama na kufungua mlango. Kabla ya kutoka nje alionekana akisema Lusifa! Lusifa!amekwashafanya roho yako kiti chake.Padri alionekana akitoka nje kwa kasi sana na Biblia yake kwapani. (uk 48-49).

Dondoo hili hapo juulinaonesha jinsi Padri alishindwa kutimiza wajibu wake katika kuhakikisha kwamba Wakristo wanamtegemea Mungu bila kukumbuka magumu wanayopitia. Kufuatia kushindwa kwa Padri ndipo Rosa alichukua uamuzi wa kujiua. Je, jamii inayomzunguka Rosa wanamwona Padri kama mtu gani? Je! Nafasi yake ameitumia ipasavyo? Hapo ndipoWakristo wanapoteza imani thabiti walionayo dhidi ya viongozi wa dini wenye dhamana ya kuongoza watu.

Vilevile kwa upande wa kitabu cha *Gamba la Nyoka*mwandishi anaonesha jinsi Padri madevu alivyokuwa akizini na mama Tinda ndio maana alikuwa akimpelekea vidonge vya uzazi wa mpango ili asijekupata mimba akaleta aibu kijijini. Kulingana na uzinzi aliokuwa anafanya, ni dhahiri kuwa watu watapoteza imani naye kama kiongozi wa dini. Mwandishi anasema:-

> Leo nimekuletea tena vidonge vingine. Vile vingine nafikiri vimekaribia kwisha. Padri Madevu alisema hali akifungua mkoba wake kutoa hivyo vidonge.  Ukiendelea kumeza

> vidonge hivi hatutapata aibu ya aina yoyote lazima tujitahidi kutunza heshima ya majina yetu Padri Madevu alisema hali akimsogelea. Hebu nifunge mlango, Mama Tinda alisema akiinuka. (uk 7)
>
> Padri Madevu ambaye alikuwa amekwishaaga mara ya pili, alisimama kwa utukufu. Mungu akubariki kwa wema na ukarimu wako unaowafanyia watumishi wake, kisha kwa mkono wa kuliaalikatakata hewa.Kwa jina la Baba, na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Alimaliza kwa sauti nzito ya kinabii. Amina.Mama Tinda alijibu bila kuulizwa akiamini dhambi zake zote zilikuwa zimeondolewa(uk 9).

Nukuu hii inaonesha kuwa Padri Madevu hakuwa mwaminifu katika kumtumikia Mungu kwani aliweza kufanya uzinzi huku akijifanya ni mtumishi wa Mungu. Halikadhalika huo ni usaliti kwa sababu huwezi kuzini halafu umalizie kwa jina la baba, na la mwana na la roho mtakatifu. Kwa mantiki hiyo ni dhahiri kwamba Wakristo wanapogundua tabia ya Padri hukosa imani na viongozi wao wa dini pamoja na kwamba wamewekwa ili waweze kuwasaidia katika masuala ya kiroho.Tukirejelea nadharia ya uhemenitiki msingi wa utukuzaji unaeleza kwamba ni jumla ya makisio mbalimbali ambayo msomaji au mhakiki huwa nayo punde aishikapo kazi yoyote ya fasihi kwa kuhusisha kiwango cha usomi na upeo wa uelewa ili kuweza kujenga hoja. Matendo ya mhusika Padri yanaonekana kuwa kinyume na matarajio ya waamini, kwani Padri ananasibishwa na Yesu kwamba matendo yake yaige mfano wa Yesu Kristo, hivyo kinyume na hapo anajenga picha mbaya kwa waamini wake.

### 4.3.2 Kurudisha Maendeleo Nyuma

Ili kuwa na jamii imara yenye ustawi hakuna budi jamii kupiga hatua katika suala zima la maendeleo. Maendeleo yanaletwa na wananchi wenyewe pale wanapoungana kwa pamoja na kuweza kutafuta namna ya kujikwamua ili kuondokana na umaskini. Mbali na hilo, viongozi wa dini nao wananafasi kubwa zaidi ya kuleta na kuhamasisha maendeleo katika ngazi ya kaya, kijiji na hata Taifa. Mwandishi ameonesha jinsi maneno ya Biblia yanavyoweza kutumiwa na viongozi wa dini katika kuhamasisha ama kukwamisha maendeleo. Padri madevu amesoma injili vizuri, lakini tafakari yake haikuendana na injili aliyoisoma badala yake anahamasisha Wakristo kupingana na mipango ya serikali. Mwandishi anasema:-

> ...alipofika mwisho watu walikaa kusikiliza mahubiri kwa makini. Padri Madevu alianza. “Wakristo wapenzi, tazameni mbele na nyuma.... Tazameni mtaona”...Mbele na nyuma kunagiza. Tazameni wenyewe. Dalili zimekwishaanza kuonekana. Mlikuwa na miji yenu na mliheshimika, sasa mnaambiwa kuhama.Mlikuwa na mangapi ambayo leo mnaambiwa si yenu- mali ya umma. Zamani watoto wenu waliwezakuwatunza, sasa hawawezi. Serikali imewanyang’anya pesa chache walizokuwa nazo. Nchi nzima watu wameinama kwa huzuni...mtahama na kuliacha Kanisa la Bwana. Mmekubali kudanganywa na wanasiasa wachache wenye njaa ya kushiba kama mbwa mwitu...mtakapoonaWachina wamejenga reli na inakwisha, jueni ukomunisti umeota mizizi... Wakristo wapenzi, kutaneni mjadili sualahili la kuhama. Mkiwa na sauti moja Mungu anaweza kuwasaidia...Kwa jina la Baba, la Mwana na la Roho Mtakatifu, Amina”.(uk 6)

Nukuu hiyo hapo juu inaonyesha jinsi mistari ya Biblia ama Kuruani ikitumiwa vibaya inavyoweza kukwamisha maendeleo ya nchi.Ukirejelea nadharia ya uhemenitiki msingi wa utukuzaji unaeleza kwamba msomaji huwa na makisio mara tu aishikapo kazi yoyote ya fasihi. Makisio hayo hujengwa na upeo wa uelewa. Padri Madevu anaonekana kutoa

tafakari ya injili kinyume na maandiko aliyosoma. Yamkini alifikiri akifanya hivyo, lengo lake la kuhamasisha Wakristo kupingana na serikali litafanikiwa.

## 4.4 Hitimisho

Katika sura hii tumechambua data na kuwasilisha matokeo ya utafiti yaliyopatikana kutokana na data za utafiti. Data za utafiti zimebaini kuwa yapo maneno ya Biblia yaliyotumiwa na mwandishi katika kufikisha ujumbe katika jamii kama vile kunyweni hii ndio damu yangu, masikini wa roho, kuungama dhambi, kiti cha enzi na picha ya mtu msalabani, damu yao na iwe juu ya vichwa vyenu, mimi nanawa mikono kama Pilato, Baba ikiwezekana kikombe hiki kinipite, kwa jina la Baba, na Mwana na la Roho Mtakatifu, na Maria, mama wa Mungu aliyezaa kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Aidha, tumejadili dhima za matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya ya Euphrase Kezilahabi kama vile kukejeli, kulea watu kiroho, kuonesha unafiki wa viongozi wa dini, na kufariji watu waliokata tamaa. Vilevile, tumeona athari za matumizi ya maneno ya Biblia kwa Wakristo. Athari hizo ni pamoja na kutokuwa na imani na viongozi wa dini pamoja na kurudisha maendeleo nyuma. Sura inayofuata ni muhtasari, hitimisho na mapendekezo.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii inahitimisha utafiti unaohusu matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka*. Sura hii imegawanywa katika sehemu kuu tatu: sehemu ya kwanza ni muhtasari wa utafiti, sehemu ya pili imefafanuza hitimisho la utafiti, na sehemu ya tatu inaeleza mapendekezo ya tafiti.

## 5.1 Muhtasari

Utafiti huu umeundwa na sura tano ambazo ndani yake kuna vipengele vidogovidogo vilivyosaidia kutimiza malengo na maswali ya utafiti. Sura ya kwanza imeshughulikia usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo na maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti pamoja na mpangilio wa utafiti.

Sura ya pili imeshughulikia mapitio ya maandiko pamoja na kiunzi cha nadharia kilichoongoza utafiti huu. Sura ya tatu imeshughulikia mbinu na namna utafiti ulivyofanyika, ikijumuisha vipengele kama vile muundo wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za ukusanyaji data, zana za utafiti pamoja na uchambuzi wa data. Vilevile udhabiti, kuaminika na maadili ya utafiti umefafanuliwa pamoja na changamoto zilizojitokeza wakati wa kukusanya data zimejadiliwa.

Sura ya nne inahusu uwasilishaji na uchanganuzi wa data ambapo vipengele kama vile matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka* vimejadiliwa. Aidha, dhima za matumizi ya maneno ya Biblia na athari za matumizi ya

maneno ya Biblia katika riwaya teule zimejadiliwa. Sura ya tano ya utafiti huu inawasilisha muhtasari wa utafiti huu, hitimisho na mapendekezo.

### 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kuwa kuna matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka.* Maneno ya Biblia yaliyobainika ni kama vile kunyweni hii ndio damu yangu, masikini wa roho, kuungama dhambi, kiti cha enzi na picha ya mtu msalabani, damu yao na iwe juu ya vichwa vyenu, mimi nanawa mikono kama Pilato, Baba ikiwezekana kikombe hiki kinipite, kwa jina la Baba, na Mwana na la Roho Mtakatifu, na Maria, mama wa Mungu aliyezaa kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

Data za utafiti huu zimebaini kuwa zipo dhima mbalimbali za matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka* za Euphrase Kezilahabi kama vile kukejeli, kulea watu kiroho, kuonesha unafiki wa viongozi wa dini, na kufariji watu waliokata tamaa. Vilevile, tumeona athari za matumizi ya maneno ya Biblia kwa Wakristo. Athari hizo ni pamoja na kutokuwa na imani na viongozi wa dini pamoja na kurudisha maendeleo nyuma.

### 5.3 Hitimisho

Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kwamba riwaya ya *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka* za Euphrase Kezilahabi, zimetumia maneno mbalimbali ya Biblia kama vile kunyweni hii ndio damu yangu, maskini wa roho, kutubu dhambi, kiti cha enzi na picha

ya mtu msalabani, damu yao na iwe juu ya vichwa vyenu, mimi nanawa mikono kama Pilato, Baba ikiwezekana kikombe hiki kinipite, kwa jina la baba, na mwana na la Roho Mtakatifu, Maria mama wa Mungu aliyezaa kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Aidha, kutokana na matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya teule, zipo dhima mbalimbali ambazo zimeweza kudhihirika kama vile kejeli, kukuza imani, unafiki wa viongozi wa dini, na kutokukata tamaa. Halikadhalika, maneno hayo yameweza kuonesha athari kwa Wakristo, ikiwa ni pamoja na kutokuwa na imani na viongozi wa dini na kurudisha maendeleo ya kiimani nyuma.

## 5.4 Mapendekezo

Sehemu hii ina vipengele viwili ambavyo ni mapendekezo kwa ajili ya uboreshaji wa utafiti na mapendekezo kwaajili ya tafiti zingine. Ni dhahiri kwamba taaluma ya Kiswahili hususani fasihi bado inauhitaji mkubwa wa kufanyiwa uhakiki na tafiti zaidi kutokana na ukuaji wake unaoambatana na mabadiliko ya sayansi na tekinolojia. Utafiti huu ulichunguza matumizi ya maneno ya Biblia katika riwaya mbili za Euphrase Kezilahabi ambazo ni *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka* ambapo, mtafiti ametimiza azma yake aliyokuwa nayo kwa kipindi kirefu kutokana na riwaya hizo kuvuta hisia za wengi kutokana na ubunifu wa kiwango cha juu na lugha iliyotumika katika kufikisha ujumbe katika jamii. Mbali na kwamba mtafiti ametimiza azma yake, yapo mapendekezo ambayo ameona yanafaa kutolewa kama ifuatavyo:-

### 5.4.1 Mapendekezo kwa Ajili ya Uboreshaji wa Utafiti

Serikali kupitia vyombo vinavyohusika na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili hususani fasihi, haina budi kuhakikisha kuwa kuwepo na utaratibu wa kutunza rekodi na vitabu vya fasihi ili isaidie katika upatikanaji wake hususani vitabu vya Kiswahili vya waandishi nguli wa Kiswahili. Hii itasaidia kuwaenzi na kuweka kumbukumbu ya maarifa ya wataalamu hawa wa fasihi. Aidha, wadau wa Kiswahili hususani walimu, wanafunzi na wahadhiri wataweza kufanya utafiti na kuweza kuboresha tafiti zilizokwisha fanywa hapo awali hususani tafiti zinazohusiana na mwandishi Euphrase Kezilahabi**.**

### 5.4.2 Mapendekezo ya Tafiti Nyingine

Utafiti mwingine unaweza kufanywa kwa kuangalia matumizi ya maneno ya Biblia katika tanzu nyingine za fasihi kama vile tamthiliya, ushairi pamoja na fasihi simulizi.

Pendekezo jingine ni utafiti linganishi. Hii ina maana kwamba utafiti mwingine unaweza kufanywa kwa kulinganisha matumizi ya maneno ya Biblia kwa waandishi wawili tofauti au zaidi; au katika vitabu ilivyoandikwa katika vipindi viwili tofauti vya mwandishi mmoja au mwandishi zaidi ya mmoja.

Aidha, utafiti mwingine unaweza kuwa katika kitabu Kitakatifu cha Koroani. Hii ina maana kwamba kuna kazi mbalimbali za fasihi andishi na simulizi zilizotumia maneno kutoka katika Koroani ambazo hazijafanyiwa utafiti. Si katika Biblia tu, utafiti mwingine unaweza kufanywa katika kuangalia matumizi ya maneno ya Koroani katika kazi za fasihi andishi au simulizi.

## MAREJEO

Babbie, E. (1999). *The Basic of Social Reseach*. Belmont: Wadworth Publishing Company.

BAKITA. (2016). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*.(Toleo la 2). Dar es Salaam: Longhorn Publishers (T) ltd.

Bryman, A. (2004). *Social Research Methods.* (Toleo la 2). Oxford: Oxford University Press.

Baradyana, J. S., na Ame, A. M. (2007). *Business Research Methods.* Dar es Salaam: Mkuki and Nyota Publishers Ltd.

Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert*. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI).Dar-es-salaam: Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam.

Cresswell, J. (2009). *Qualitative, Quantitative & Mixed Methods Approches*. (Toleo la 3). Lons Angeles: SAGE Publications.

Denscombe, M. (1998). *The Good Research Guide: For Small Scale Social Reserch Projects*. Buckingham: Open University Press.

Frenkel, G. (1998). *Qualitative Research Techniques*. London: Cambridge University Press.

Gadamer, H. (1960). "Gadamer's Hermeneutic Contribution to a Theory of Time-Conciousness". http: //www.ajol.info. Imepakuliwa tarehe 17-03-2019.

Ighondo, P. (2019). "Utatu Mtakatifu". http://www.vaticannews.va. Imepakuliwa tarehe 03-09-2019.

Jonker, J. na Pennink, B. (2010).*The Essence of Research Methodology*: *A Concise Guide for Masters & Ph.D students in Management Science*. Neitherland: Springer.

Kezilahabi, E. (2015). *Rosa Mistika*.(Toleo la 2). Nairobi: Kenya Literature Bureau.

———— (2015). *Gamba la Nyoka.* (Toleo la 2). Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

Njogu, K na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New age International (p) Ltd.

__________ (2008).*Research Methodology: Methody and Technique*(2nd Revised). New Delhi: New age International Publishing Ltd.

__________ (2009). *Research Methodology: Methods and Techniques* (2nd Revised Ed.). New Delhi: New Age International Publishers Ltd.

Koul L. (2006). *Methodology of Educational Research.*( Toleo la 4). New Delhi: Vikas Publishing House.

Mfinanga. M. (2017). "Uajinabishaji wa Motifu ya Kifo katika riwaya ya RosaMistika, Kichwa Maji, Gamba la Nyoka na Dunia Uwanja wa Fujo".Tasnifu ya Uzamili. (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

Mlaga, W. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne 21*Dar es Salaam. Heko Pulbishers Ltd.

Mligo, E. (2012).*Jifunze Utafiti: Mwongozo Kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti Yenye Mantiki*. Dar es Salaam: Ecumenical Gathering.

Msangi, E. (2018). "Ubiblia katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo". Tasnifu ya Uzamili. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Msokile, M. (1992). *Kunga za fasihi na Lugha*. Dar-Es-Salaam: Educational Publishers.

Madumulla, J. (2009). *Riwaya ya Kiswahili, Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi.*Dar es Salaam: Mture Educational Publishers LTD.

Malugu, A. (2015). "Nafasi ya Fasihi katika Kusawiri suala la Dini". http://www.ajol.info Imepakuliwa 17-03-2019.

Materu, M. L. (1976). "Fani ya Hadithi na Riwaya" Katika Kioo cha Lugha. Juz 72.

Marisya, P. (2017). "Mchango wa Sajili ya Kidini katika kufanikisha riwaya mbili za Ken Walibora: Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi". http://www.erepository.uonbi.ac.ke Imepakuliwa tarehe 16- 03- 2019.

Makhino, N. (2017). "Ukanushi-udhanaishi wa Rosa katika riwaya ya Rosa Mistika". Tasnifu ya Uzamili. (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Makumira.

Mulokozi, M. (1996).*Fasihi ya Kiswahili*. Dar Es Salaam: Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Mosha, P. (2013)."Usawiri wa mhusika Padri katika riwaya za Euphrase Kezilahabi: Uchunguzi katika *Rosa Mistika, Gamba la Nyoka* na *Nagona"*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.

Nsebemuki, L. (2004). *Msingi wa Maarifa ya Utafiti*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Omari, C.K. na Mvungi, M. (Wah.) (1981). *Urithi wa Utamaduni Wetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Padgett, D. (2004). The Qualitative Research Experience. America: Wadsworth/ Thomson Learning.

Pembe, H. (Ht) "Majina ya Wakristo nchini Tanzania". Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.ND Jounal halijatoka rasmi hadi sasa.

Ponera, A.S. (2010). "Ufutuhi katika Nathari za Kiswahili: Ulinganisho wa Nathari za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi". Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Ranganatham, M. na Krishnaswami, O. (2010). *Methodology of Research in Social Science*, Bangalore: Himalaya Publishing House.

Rehak, V. (2007). Kazimoto and Meursault: "Brothers in Despaire and Lonileness. Comaring Kezilahabi's Kichwamaji and Camus' L"Etranger. Katika Swahili Forum 14: 135-151.

Sakkos, T. (2008). *"An Alienated intellectual" Rereading E. Kezilahabi's Novel Kichwamaji*. katika Nordic Journal of African Studies 176-190.

Senkoro, F.E.M.K.(2011).*Fasihi Andishi*. Dar es Salaam: Kauttu Ltd.

———— (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar-es-Salaam: Dar-Es-Salaam Press and Publicity Centre.

———— (1976). "Utamaduni katika Riwaya ya Kiswahili" Katika *Kiswahili* Juz. 46/2 uk 74-94.

Tromp, D. na Kombo D. (2006). *Proposal and Thesis Writing*. Nairobi: Pauline's Publications Africa.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*:Nairobi: Phoenix Publisher Ltd.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi na Istilahi na Nadharia*. Nairobi: FocusPublications.

Wanjala, F. S. (2012). *Kitovu cha Fasihi Simulizi kwa Shule, Vyuo na Ndaki*. Mwanza: Serengeti Bookshop.